

UHAKIKI KISEMANTIKI WA LAKABU ZA EKEGUSII

MILCAH NYATHIRA

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA LUGHA,
ISIMU NA FASIHI ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI (KISWAHILI) YA CHUO KIKUU
CHA KISII KENYA.

SEPTEMBER

2021

UNGAMO NA IDHINI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo chochote kwa mahitaji ya shahada yoyote.

.....

Nyathira Milcah

Nambari ya usajili; MAS16/60248/15

Tarehe.....

IDHINI

Kazi hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo kikuu cha Kisii.

.....

Tarehe.....

Dkt. Opande Nilson Isaac

Idara ya lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu Cha Kisii

.....

Tarehe

Dkt. Moochi Nyandoro Charles

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu Cha Kisii

HATIMILIKI

Kazi hii hairuhusiwi kutolewa kwa namna yoyote ile, yote au sehemu isipokuwa kwa matumizi ya kitaaluma ya utafiti, kujisomea na kurejelea kwa kibali kutoka kwa mkurugezi wa masomo ya uzamili kwa niaba ya mwandishi na chuo kikuu cha Kisii.

TABARUKU

Kwenu nyinyi wazazi wangu wapendwa: Babangu James Gitau (Maarifa) na mamangu Jane Agosa, mkajinyima ili kunisomesha, mkanielekeza na kunipa mizungu ya kukabili changamoto za maisha.

Kwenu nyie ndugu zangu wapendwa, watoto wangu, mume wangu na wote wanaonitazama kama kielelezo bora. Kumbukeni 'Inawezekana'.

SHUKURANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunipa nguvu za kukabiliana na vizingiti mbalimbali wakati wa kutafitia mada hii. Hamu na ilhamu aliyonipa Mungu ilinitia mshawasha wa kuisukuma mbele kazi hii.

Pili, naishukuru tume ya kuajiri walimu kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu. Pia nawatolea shukrani za dhati wasimamizi wangu, Dkt. Opande Nilson Isaac na Dkt. Moochi Nyandoro Charles kwa msaada wenu wa kupigiwa mfano. Pale nilielekea kupoteza mwelekeo mlinisahihisha kwa ufaafu. Mchango wenu nitauthamini daima. Mlinivumilia na kunihimiza nitie bidii ili kuukamilisha utafiti huu mintarafu ya mpango wa muda uliotengwa. Mlinifunza mengi sio tu katika utafiti huu bali pia katika maisha kwa ujumla. Mungu awape mbawazi njema.

Aidha, nawashukuru sana Dkt. Sawe George, Mzee Peter Nyamache na wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Kisii, ushauri na maelekezo niliyoyapata kutoka kwenu yalinitia ukakamavu maishani na kuuathiri mwonoulimwengu wangu wa maisha kichanya. Shukrani jazila.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI	ii
HATIMILIKI	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKURANI	v
YALIYOMO	vi
ABSTRACT	viii
IKISIRI.....	ix
SURA YA KWANZA.....	1
MISINGI YA UTAFITI.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa utafiti	1
1.3 Suala la utafiti	5
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	5
1.5 Maswali ya utafiti.....	5
1.6 Sababu ya kuchagua mada na Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.7 Upeo na mipaka ya utafiti	7
1.8 Misingi ya nadharia	7
SURA YA PILI	11
MAPITIO YA MAANDISHI.....	11
2.1 Utangulizi.....	11
2.2 Maana ya lakabu.....	11
2.3 Mbinu mbalimbali za kubuni lakabu.....	12
2.4 Matumizi ya lakabu katika jamii	14
SURA YA TATU	18
MUUNDO NA UTARATIBU WA UTAFITI.....	18
3.1 Utangulizi.....	18
3.2 Muundo wa utafiti.....	18
3.3 Eneo la utafiti	18
3.4 Washiriki wa utafiti	19
3.5 Uteuzi wa sampuli.....	20
3.6 Ala na mbinu za kukusanya data	20
3.6 Maadili ya kiutafiti	21
SURA YA NNE	22

UWASILISHAJI NA UHAKIKI WA DATA	22
4.1 Utangulizi.....	22
4.2 Maana ya lakabu teule za EkeGusii za wachezaji kandanda	23
4.2.1. Lakabu za maumbile na rangi	27
4.2.2.Lakabu zinazowasilisha sifa mbalimbali	33
4.2.3 Lakabu za wanyama wa mwituni, wanaofugwa na wa majini	39
4.2.4 Lakabu za wadudu na ndege	43
4.2.5 Lakabu za mimea	46
4.2.6 Lakabu zinazoonyesha matendo fulani.....	48
4.2.7 Lakabu zinazorejelea vitu mbalimbali.....	50
4.2.8 Lakabu za sehemu mbalimbali	55
4.3 Mbinu zinazotumika kuunda lakabu	56
4.3.1 Uundaji wa lakabu kutokana na nomino mbalimbali	57
4.3.2 Uundaji wa lakabu kutoka kwa vitenzi	63
4.3.3 Muundo wa sentensi	64
4.3.4 Lakabu zinazoudwa kutokana na mbinu ya ukopaji	64
4.3.5 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya ufupishaji.....	65
4.3.6 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya uradidi.....	65
4.3.7 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya uambatanishaji.....	66
4.3.8 Uundaji wa lakabu kwa kutumia mbinu ya uhamishaji	66
4.4 MATUMIZI YA LAKABU KATIKA MCHAKATO WA KUCHEZA KANDANDA	67
SURA YA TANO	75
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	75
5.1 Utangulizi.....	75
5.2 Hitimisho.....	75
5.3 Masuala yanayohitaji tafiti zaidi	80
MAREJEO	81

ABSTRACT

Considering that nicknames are common in our daily communication, they are very important concepts in establishing or destroying relationships in the society. This study aimed at achieving the following objectives: First of all, to distinguish meaning of EkeGusii nicknames used by soccer players. Secondly, to elucidate various methods used in forming EkeGusii nicknames used by soccer players and lastly, to elaborate the uses of EkeGusii nicknames in the whole scenario of a soccer match. To achieve these objectives, the research was guided by the frames tenet of the Frames Semantic theory. This tenet was used to explain how meanings are cognitively retrieved from the speakers' mental encyclopedic knowledge. The study outlined various methods used in forming and classifying EkeGusii nicknames and brought out types of meaning present in EkeGusii nicknames. The descriptive research design was applied in the study to render an analysis of EkeGusii nicknames used by soccer players in Kenyena sub-county, Kisii county, Kenya. Primary data was collected through oral structured interviews whereas secondary data was collected from selected works in the library. Those interviewed orally were soccer players and their fans who were selected randomly. Data was analysed by use of tables and Frames. Frames were particularly used to define concepts that guided the retrieval of meanings. The study concluded that soccer players have nicknames which are meaningful and have semantic values: cognitive and connotative meanings that are governed by the motive of the creator of the nickname and the settings or situation of the one being referred by the nickname. These nicknames are created using various methods including word derivation, reduplication, compounding, repetition. The research also examined the importance of using nicknames in a whole scenario of a soccer match and concluded that nicknames were very important because they capture the perception of the fans about how the players are playing so that they can improve or change their playing tactics. The research shows that EkeGusii nicknames of soccer players are embedded with lot of teachings about the traditions of the AbaGusii people and also their stand on issues about gender, agriculture, livestock farming and their cultural norms in general.

IKISIRI

Lakabu hutumika sana katika mawasiliano baina ya wanajamii hivyo basi ni kiungo muhimu sana katika kufafanua mahusiano hasi au chanya baina ya wanajamii. Utafiti huu ulishughulikia madhumuni mahususi yafuatayo: Kwanza, kubainisha maana za lakabu za lugha ya EkeGusii za wachezaji wa mchezo wa kandanda. Pili, kufafanua mbinu mbalimbali zinazotumiwa kubuni majina ya lakabu ya EkeGusii na tatu, kuchanganua umuhimu wa lakabu hizi katika mchakato wa mchezo wa kandanda. Ili kufikia malengo haya, utafiti huu ulielekezwa na mihimili ya nadharia ya semantiki ya fremu inayoeleza kuwa maana hupatikana kutokana na maarifa ya siku nyingi yaliyohifadhiwa kwenye ubongo wa binadamu. Utafiti huu ulifanyika katika kaunti ndogo ya Kenyena iliyoko katika kaunti ya Kisii nchini Kenya. Huu ulikuwa ni utafiti wa kimaelezo. Data ya kimsingi ilikusanywa nyanjani kupitia mahojiano ya moja kwa moja. Mahojiano haya yaliongozwa na maswali teule yaliyolenga kuibua hisia lengwa. Watafitiwa walikuwa wachezaji kandanda na mashabiki sugu waliochaguliwa bila kufuata utaratibu maalumu. Data nyingine zilikusanywa maktabani kwa kuzingatia kazi teule zilizohusiana na utafiti. Nadharia ya fremu ilitumika kueleza namna maana hutambuliwa na kustawishwa kutokana na maarifa yaliyomo kwenye akili ya msemaji. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa maelezo na majedwali yaliyoelekeza na kudhihirisha uchanganuzi wa semantiki za lakabu husika. Fremu zilitumika kufafanua dhana zilizoongoza ustawishaji wa maana ya majina ya lakabu za EkeGusii zinazopewa wachezaji wa mchezo wa kandanda. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa wachezaji kadanda wana lakabu ambazo zina dhana ya kisemantiki: maana tambuzi na ashirifu inayotokana na kichocheo cha utunzi wa lakabu hiyo na mandhari au hali ya anayerejelewa na lakabu fulani na hubuniwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile unominishaji wa vitenzi, utohozi, ukopaji, uradidi, ufupishaji na uhamishaji wa maana. Utafiti pia ulichunguza umuhimu wa kutumia lakabu katika mchakato wa kucheza kandanda na kubaini kuwa lakabu huwasaidia wachezaji kandanda kuelewa msimamo wa mashabiki kuhusu namna wanacheza mchezo wao ndiposa waweze kujibidiisha zaidi. Utafiti umeonyesha kuwa lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda hushamiri mafunzo kuhusu mila na tamaduni za AbaGusii pamoja na misimamo yao kuhusu maswala ya jinsia, kilimo, ufugaji, na maadili kwa jumla.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Sura hii ya kwanza inaeleza usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na pia misingi ya nadharia iliyotumika katika utafiti.

1.2 Usuli wa utafiti

Lakabu ni jina msimbo au jina la kupanga ambalo mtu hujibandika au hubandikwa kutokana na sifa zake za kimaumbile, kitabaka, kitabia, kinasaba au kimatendo. Aghalabu, lakabu huwa ni neno moja au fungu la maneno lililo na maana fiche au ya kiistiari (Matei, 2011). Sifa mojawapo ya lakabu ni kuwa, ingawa sio jina halisi la mtu, huweza kudumu na kulifanya jina halisi la mtu huyu kusahaulika. Mackay (1980) anasema kuwa majina ya lakabu ni majina ambayo mtu hupokea ili kuongezea majina yake halali.

McDowel (1981) anasema kuwa matumizi ya majina ya lakabu hudhibitiwa na utamaduni wa jamii husika. Matumizi ya majina ya lakabu ni jambo ambalo limekuwa la kawaida katika jamii. Upo uwezekano kwamba kila mtu mzima ana jina la lakabu au alikuwa amepewa jina hilo wakati alipokuwa akikua. Pindo (2017) anaeleza kuwa wakati mwingine majina haya huwa siri kiasi kwamba anayerejelewa hana mwao kwamba ni yeye anayezungumziwa. Pia, anaeleza kuwa majina ya lakabu ya kabila la Acholi nchini Uganda hutumika kuhifadhia na kupasha habari kutoka kizazi kimoja hadi kingine .

Maina (2015) anasema kuwa sisi kama wanadamu tuna tabia ya ‘kuwabatiza’ wenzetu majina ya lakabu kiholelaholela kwa minajili ya mawasiliano baina yetu. Majina haya ya lakabu yanaweza kutokana na maumbile, siha, au hata kazi mbalimbali wanazozifanya watu katika jamii. Wakati mwingine mtu anaweza

kutamka neno au maneno visiyo katika mazungumzo yake na huo ukawa mwanzo wa jina lake la lakabu. Nchini Kenya kuna uhuru wa kujieleza na hivyo basi watu wengi hawaoni tatizo kuwapa wenzao majina ya lakabu bila kujali hadhi zao katika maisha. Ni kutokana na hali hii ambapo utapata hata kiongozi wa nchi amepewa majina mbalimbali ya lakabu kudhihirisha kuwa hakuna yeyote ambaye ameachwa nyuma kuhusiana na suala hili la lakabu. Hivyo basi ni dhahiri kuwa hakuna mtu anayeweza kuepuka kupewa jina la lakabu ambalo anaweza kulipenda au hata kulichukia milele.

Kuna watu ambao majina ya lakabu yamewasaidia sana kubadili hali yao ya maisha hata kuwafanya kuamua kuhalalisha majina haya ya lakabu ili yawe majina yao halisia. Katika siasa Wainaina (2013) anatoa mifano mitatu ya wanasiasa ambao majina ya lakabu yaliwasaidia sana kufaulu katika vinyang'anyiro mbalimbali vya kisiasa katika uchaguzi wa mwaka wa elfu mbili na kumi na tatu katika mkoa wa Kati. Wanasiasa hawa waliamua kuhalalisha majina ya lakabu waliyokuwa wamepewa na wananchi kutokana na majukumu mbalimbali waliyokuwa wametekeleza katika jamii. James Mathenge Simion kwa mujibu wa Wainaina (2013) ni mwanasiasa ambaye alifaidika sana katika siasa kwa sababu ya kutumia jina lake la lakabu ambalo ni *Kanini Kega* (mdogo mzuri) Gavana Francis Mwangi aliamua kutumia jina lake la lakabu la *Mwangi wa Iria* ili kumtofautisha na mpinzani wake mkuu ambaye aliitwa daktari Mwangi. Kimani Paul kwa mujibu wa Wainaina (2013) ni mwanasiasa aliyefaidika sana kwa kutumia jina lake la lakabu *Matangi* katika siasa. Jina hili la lakabu lilimpa umaarufu na kumwezesha kumpiku mpizani wake mkuu bilionea Bwana Githunguri. wapinzani wake wengine wote kwa pamoja wakipata chini ya kura elfu mia moja. Wanasiasa wengine waliohalalisha majina yao ya lakabu kuwa majina yao halali ni kama vile Mheshimiwa Fedinard Waititu, *Baba yao* ambaye alikuwa gavana wa kaunti ya Kiambu na Mheshimiwa Mbuvi, *Sonko* ambaye alikuwa gavana wa kaunti ya Nairobi. Kazi hii ya Wainaina (2013) ni dhahirisho kuwa majina ya lakabu huwa ni muhimu sana yanapotumiwa ikilinganishwa

na majina halisi ya mtu hivyo kuchochea utafiti huu wa sasa uliolenga kuhakiki maana na umuhimu wa matumizi ya lakabu za EkeGusii katika mchakato wa mchezo wa kandanda.

Ibukuni (2014) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya majina ya lakabu katika chuo kikuu cha Nigeria anaeleza kuwa wanafunzi wengi wa vyuo vikuu hubadili majina yao wenyewe na kujipa majina ya lakabu pale ambapo wanahisi kuwa majina yao halisi hayawapi sifa au hayawasaidii kujitambulisha namna wapendavyo. Utafiti huu wa sasa ulichunguza pia iwapo wachezaji wa kandanda hujipa majina ya lakabu wao wenyewe au hupewa na sababu za kujipa au 'kubatizwa' majina haya. Hata hivyo, utafiti huu wa sasa ulitofautiana na huo wa Ibukuni (2014) aliyejishughulisha na kuangalia sababu za wanafunzi kujipa majina ya lakabu kwani ulichambua mbinu za lugha zinazotumika kubuni lakabu hizi na pia kuangalia semantiki ya lakabu hizi.

Utafiti unaokaribiana na huu ni utafiti alioufanya Adetunji (2009). Katika utafiti huo mtafiti alitafiti kuhusu majina ya lakabu ya kiyoruba yanayopewa wachezaji soka wa ligi kuu ya uingereza, kwa mfano, timu ya Chelsea, Arsenal, Manchester United na Liverpool. Utafiti huo ulionyesha namna majina ya lakabu yaliyopewa wachezaji wa ligi kuu ya uingereza yanavyoonyesha mila na tamaduni za Wayoruba na pia sehemu ya kijigrofia waliomo mashabiki hao wa mpira. Utafiti huo wa Adetunji (2009) hukuongozwa na nadharia yoyote kinyume na utafiti huu wa sasa ambao uliongozwa na nadharia ya Kisemantiki ya Fremu. Pia, utafiti huu wa sasa uliainisha lakabu kwa kurejelea muktadha wa masuala ya kijamii na pia kwa kurejelea mtazamo wa kiisimu ili kubainisha maana zinazojitokeza.

Utafiti mwingine unaohusu majina ya lakabu ni utafiti wake Candrea (2001) ambaye alifafanua lakabu kama maneno yanayotumiwa na watu kukonyoa tabia mbovu za mtu. Utafiti wake Candrea (2001) ulionyesha kuwa ni wasifu hasi pekee unaostahili kubuniwa lakabu mwafaka. Bila shaka hatuwezi kujifunga katika matumizi ya lakabu kuwa utambuzi wa wasifu pekee; Hivyo basi, utafiti huu wa semantiki ya lakabu za EkeGusii zinazopewa wachezaji wa mpira wa kandanda ulikusudia kuainisha

matumizi yote ya majina ya lakabu hizi ikiwemo namna zinavyohalalisha tabia za watu na zinavyokashifu wasifu hasi unaotokana na maumbile na hata matendo ya mtu.

Felecan (2009) ni mtafiti mwingine aliyeshughulikia masuala ya lakabu. Katika utafiti wake (Felecan, 2009) alitafiti mawasiliano ya lakabu na kupambanua lakabu hizi katika makundi mbalimbali kutokana na thamani zao za semantiki. Pia, alionyesha namna baadhi ya lakabu zilivyoibuka katika jamii ya Warumi na namna zilivyoathiri mahusiano na maisha ya waliopewa lakabu hizi. Kazi hii ya Felecan (2009) ilikuwa dira katika upambanuzi wa majina ya lakabu ya EkeGusii. Hata hivyo, kazi hii ya Felecan (2009) haikushughulikia semantiki ya lakabu, mbinu zilizotumika kukusanyia data, utamaduni wa jamii husika na pia dhana zilizotumiwa kutambua maana za lakabu zilizotumika. Masuala haya ndiyo yaliyopewa kipaumbele katika uchanganuzi wa majina ya lakabu ya lugha ya EkeGusii yanayopewa wachezaji wa mpira wa kandanda katika kaunti ndogo ya Kenyena.

1.3 Suala la utafiti

Majina ni muhimu sana katika jamii yetu kwani ni njia ya u(ji)tambushaji. Majina hudhihirisha watu, mahali na vitu. Majina hasa ya lakabu hutumika katika mawasiliano baina ya wanajamii na hivyo basi ni kiungo muhimu sana katika kufafanua mahusiano hasi au chanya baina ya wanajamii. Kila mtu anaweza kujipa jina la lakabu au akapewa jina hilo na wanajamii bila kujali iwapo atalipenda jina hilo au la. Hata hivyo, lakabu zinapuuzwa hivyo hazifanyiwi utafiti toshelevu kuonyesha ni kwa nini zinatumiwa. Matumizi ya majina haya ya lakabu yanaweza kuzua mtafaruku na uhasama baina ya watu hasa wakati mtu anatomia jina la lakabu ambalo linamkera anayerejelewa. Ili kuepuka mtafaruku huu kuna haja ya kutafiti majina haya ya lakabu na kuweka wazi maana yake. Utafiti huu wa lakabu za Ekegusii zinazotumiwa na wachezaji wa kandanda ni jaribio la kuhakiki semantiki na sifa za lakabu. Pia unaangazia namna lakabu hizi hubuniwa huku ukionyesha namna vipengele vya kitamaduni na kijamii vinapambanua maana tambuzi na maana ashirifu ya majina ya lakabu kwa kurejelea mihimili ya nadharia ya kisemantiki ya fremu.

1.4 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kuafikia madhumuni mahususi yafuatayo:

- I. Kubainisha maana ya lakabu za Ekegusii zinazotumiwa na wachezaji kandanda.
- II. Kufafanua mbinu mbalimbali za lugha zinazotumiwa kubuni lakabu za lugha ya EkeGusii za wachezaji kandanda.
- III. Kupambanua matumizi ya lakabu za EkeGusii katika mchakato wa mchezo wa kandanda.

1.5 Maswali ya utafiti

Maswali yafuatayo ndiyo yaliyoongoza utafiti:

- I. Ni nini maana za lakabu za lugha ya EkeGusii zinazotumiwa na wanakandanda?
- II. Majina ya lakabu hubuniwa vipi?
- III. Je, lakabu hutumiwa vipi katika mchakato wa mchezo wa kandanda?

1.6 Sababu ya kuchagua mada na Umuhimu wa Utafiti

Suala la matumizi ya majina ya lakabu katika jamii huhusu mtoaji wa jina na mpokezi wa jina hilo. Wakati mwingine mtu anaweza kujibandika jina au hata akabandikwa jina kiasi cha watu kusahau jina lake asilia. Wakati mwingine wanajamii wanaweza kumpa mtu jina la lakabu ambalo atalipenda au hata wakampa jina ambalo hata hana habari kuwa ni lake mradi tu wao wafanikishe mawasiliano yao. Hivyo basi majina ya lakabu ni ya maana katika jamii kama yalivyo majina mengine ya kijamii. Hata hivyo, kama anavyoeleza Holland (1990) ni tafiti chache sana zilizofanywa kuhusiana na suala hili la majina ya lakabu. Tafiti zilizofanywa kuhusiana na masuala ya majina ya lakabu hasa nchini Kenya ni chache mno. Makala machache yaliyoandikwa kuhusu masuala ya majina ya lakabu ni finyu mno na hayatoshi kufafanua suala lote la majina ya lakabu. Hivyo utafiti huu ulikusudiwa kukusanya na kuhifadhi maelezo ya kiisimu kuhusu majina ya lakabu katika lugha ya EkeGusii.

Sajili ya michezo hasa mchezo wa kandanda husisimua na kuwachangamsha watu wengi katika jamii. Hali hii hushadidisha haja ya kufanyia utafiti sajili hii na hasa kutathimini vigezo vya kubuni lakabu na ufaafu wa lakabu hizi zinazotumika katika muktadha wa mchezo wa kandanda. Aidha, utafiti huu utasaidia kujenga na kuboresha nadharia ya Semantiki ya Fremu. Mihimili ya nadharia hii ndio iliyoongoza utafiti huu kisha kusaidia kuifafanua zaidi.

Kulingana na ruwaza ya Kenya ya mwaka wa elfu mbili na thelathini (2030), mbali na kwamba inatambua sera ya taifa ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kuwa rasmi, imeweka pia hamasa katika uendelezaji wa

lugha za kiasili nchini Kenya kwa kuhimiza zifanyiwe utafiti wa masuala mbalimbali ya kiisimu, fasihi na utamaduni wa lugha hizi kufafanuliwa na kuwekwa bayana. Utafiti huu ulitarajia kuweka wazi maswala ya kiisimu ya lugha ya EkeGusii ambayo ni mchango mkubwa katika isimu ya lugha za Kenya na Afrika kwa jumla. Utafiti huu pia unaruhusu uratibu na uhifadhi wa makala ya kiusomi kuhusu lugha ya EkeGusii. Nash (2009) anasema kuwa EkeGusii ni miongoni mwa lugha ambazo hazijatafitiwa kwa uketo. Utafiti huu utawafaa wanajamii kwani wanaathiriwa kwa njia moja au nyingine na masuala yanayohusu majina ya lakabu.

1.7 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kudhihirisha maana (maana tambuzi na maana ashirifu), mbinu zilizotumika kuunda lakabu za EkeGusii na matuizi ya lakabu ya EkeGusii katika mchakato wa mchezo wa kandanda pekee. Utafiti huu ulifanyika katika jimbo dogo la Kenyenyema kwa kuwa kuna michuano mingi ya kandanda ambayo hufanyika huko. Utafiti huu ulijikita katika lakabu za wanakandanda wa kiume pekee. Utafiti huu ulishughulikia lakabu za EkeGusii za wachezaji wa mchezo wa kandanda pekee.

1.8 Misingi ya nadharia

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Kisemantiki ya Fremu inayoeleza namna tunavyotambua maana ya majina kutokana na elimu aliyonayo mtu kupitia matumizi ya dhana zinazohusiana. Elimu ni habari azijuazo mtu kuhusu majina haya ya lakabu. Nadharia ya Fremu ni nadharia tambuzi inayosawiri ulimwengu halisi (Sebastian, 2014) iliyozuka miaka ya sabini. Waasisi wake ni Charles Fillmore, George Lakoff, Ronald Langacker, Leonard Talmy, na Evans Thomson. Kulingana nao, dhana ya neno inaweza kueleweka kwa kurejelea vielelezo vilivyomo akilini mwa mtu ambavyo

vinatokana na uzoovu wa siku nyingi. Kulingana nao, maana hutokana na maarifa yaliyohifadhiwa katika akili kwa muda mrefu. Maarifa haya ndiyo hutumika kufafanua dhana hapo baadaye.

Fillmore (1985) anaeleza kwamba nadharia ya Semantiki ya Fremu hujaribu kufafanua maana ya neno kwa kulihusisha neno hilo na usuli wake kwa jumla. Lugha huonyesha utamaduni wa jamii hivyo basi inaweza kueleweka kwa kurejelea upataji wa lugha fulani na pia michakato kwenye akili ya mtu. Fremu ilitumika katika utafiti huu kuhushisha ujuzi wa utamaduni na dhana akilini. Nadharia ya Semantiki ya fremu inashikilia kuwa maana huoana na mandhari (Fillmore,2001). Hivyo basi, maana inaweza kudhihirika kutegemea usuli au mandhari. Mihimili ya nadharia ya semantiki ya fremu ndiyo iliyotumikakatika utafiti huu. Fremu ni mkusanyiko wa habari kuhusu hali fulani ambayo imehifadhiwa katika akili ya binadamu. Matamshi ya kiisimu huathiriwa na vipengele mbalimbali vinavyosimamiwa na fremu inayoangaziwa. Kwa mujibu wa Fillmore (1985) fremu ni mfumo wa dhana ambazo zinahusiana kiasi kwamba ili kuelewa moja ya dhana hizi inakubidi kuelewa mfumo mzima unaohusishwa na dhana inayotajwa. Wakati mojawapo ya vipengele katika mfumo huu inapojadiliwa katika matini au mazungumzo vipengele vyote katika mfumo huu hujidhihirisha wazi. Keith (2001) anaongezea kuwa vipengele katika mfumo huu vimefungamana ili kuunda muundo unaoeleweka kwa kurejelea tajiriba ya muda mrefu. Tafiti za semantiki za fremu huhusu utambuzi wa fremu mbalimbali, wajibu wa semantiki wa kila mandhari inayojitokeza katika kila fremu, na namna fremu mbalimbali zinavyohusiana. Fillmore (1985) anatumia mifano ifuatayo ili kufafanua fremu.

I. Natamani kutua ardhi

II. Natamani kufika nchi kavu

Hata ingawa maneno haya mawili, ardhi na nchi kavu, yanarejelea kitu kimoja, sentensi ya kwanza inaashiria mzungumzaji aliye angani (kwenye ndege) nayo sentensi ya pili inaashiria mzungumzaji aliye

majini. Hivyo basi ardhi inaeleweka ndani ya fremu ya usafiri wa angani na ndani ya fremu hii ardhi ni kinyume cha angani ilhali nchi kavu inaeleweka katika fremu ya usafiri wa baharini na ndani ya fremu hii nchi kavu ni kinyume cha baharini. Katika mfano huu fremu imefungwa katika hisia za maneno ardhi na nchi kavu. Kupitia kwa hifadhi ya mgao wa maarifa ajuayo mtu, ufafanuzi wa hali mbalimbali hufanyika kwa kurejelea fremu inayofaa hata kama maneno yaliyotumika sio wazi.

1.8.1. Sababu ya kuchagua mhimili wa fremu

Kama nadharia ya isimu tambuzi, nadharia ya semantiki ya fremu huchunguza lugha na kuihusisha na vitengo mbalimbali vya viziada lugha kama vile maarifa na tajriba ambayo huathiri namna inavyoeleweka. Fillmore (2001) anafafanua kuwa katika nadharia ya semantiki ya fremu, neno huwasilisha kategoria ya tajriba: mojawapo ya madhumuni ya utafiti huu ilikuwa ni kuchambua sababu zilizopelekea jamii lugha kuunda kategoria zilizowasilishwa na neno na kuongezea sababu zilizochangia katika ufafanuzi wa maana ya neno. Hivyo haya yalifaa sana katika uchanganuzi wa maana ya majina ya lakabu kwani yalisaidia kuhusisha jina la lakabu katika jamii na kirejeshi cha tajriba katika ulimwengu halisi wa mzungumzaji ambao ni sehemu ya maarifa. Akili huwa na kazi muhimu sana ya kufafanua vipengele vya msamiati na hata maumbo makubwa. Maarifa kuhusiana na kilichotajwa yalisaidia kufumbua dhana zilizoelekeza kufafanua namna lakabu mbali mbali zilivyobuniwa. Uwezo wetu tambuzi (wa kiakili) ulirahisisha fasili ya kila msamiati kila tulipokumbana na neno kwa mara ya kwanza. Baadhi ya fremu zilitangamana ilihali fremu zingine zilikuwa chini ya fremu zingine zile kubwa. Wakati jina la pekee lilipotajwa (lakabu), mawazo ambayo ni kama mandhari yalijitokeza akilini kuhusiana na maana na matumizi yake na hiyo kusaidia kupambanua athari za matumizi ya lakabu za lugha ya EkeGusii katika mchakato wa mchezo wa kandanda.

Luhrer na Kittay (1992) wanasadikisha umuhimu wa matumizi ya nyanja na viunzi (fremu) katika uchanganuzi wa maana ya majina. Kwani kila kiunzi au miliki (kwa mfano lakabu) huwa na mfumo tofauti

wa majina pia maana ya majina ya pekee huwa na uhusiano na jina hilo husika. Hivyo basi majina yaliyotokana na nomino za kawaida au jumla yalitarajiwa kuwa na sifa bainifu za kisemantiki zilizojitokeza wazi kupitia kwa viunzi

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha yaliyoandikwa na watafiti wengine kuhusu maana ya lakabu, mbinu zinazotumika kuvumbua lakabu na matumizi ya lakabu katika jamii.

2.2 Maana ya lakabu

Lakabu ni majina ya kuchekeka au kukejeli yanayojulikana na yanayotumika kumrejelea mtu fulani badala ya jina lake kamili (Koopman, 2002). Lakabu ni mojawapo ya vipera vya utanzu wa semi katika fasihi simulizi ingawa hakika hujitokeza katika tanzu na vipera vingine vingi kama vile sifo, malumbano ya utani na majigambo. Kwa mujibu wa kamusi mtandaoni ya Oxford, jina lakabu lilijitokeza katika mwaka wa elfu moja mia tatu na tatu likiwa na maana ya jina (kwa kawaida jina linalo fahamika au la kuchekeka) linalopewa mtu, mahali na kadhalika kama jina mbadala au jina la kuongezea jina halisi. Lakaw (2006) anafafanua etimolojia ya jina hili kuwa “*Eke- name*’ kumaanisha jina lingine. Anaongezea kuwa katika karne ya kumi na tano jina “*Nickname*” lilirasimishwa kama kisawe cha “*Eke name*” yaani lakabu. Hivyo basi kuashiria kuwa majina ya lakabu huwa hayafuati mfumo wa kawaida unaotumiwa kuwapatia watoto majina asilia.

Kwa mujibu wa Mlokozi (1989) majina haya ya lakabu huwa na vigezo mbalimbali. Katika kigezo cha umbile na tabia lakabu inayohusika hutumia maneno yenye maana iliyofungwa na sitiari. Phafoli (2009) anaeleza kuwa majina ya lakabu wapewayo au wajipayo wasanii wa nyimbo kule Bosotho hutokana na vipengele mbalimbali vikiwemo rejimenti, wajumbe na sehemu anakotoka msanii huyu. Majina ya lakabu

huwa na mhusika anayepewa sifa na anayetoa sifa zenyewe. Lakabu huwa na matini inayobadilikabadilika na hivyo ni sanaa inayopita. Lakabu hufuata watu, mahali na wakati.

Lakabu huwa sio rasmi; ni kwa nadra sana unaweza kupata lakabu zikiwa zimeandika katika vyeti rasmi kama vile hati za kuzaliwa, vyeti vya shule, vyeti ya kuendesha gari na kadhalika. Kahari (2009) anaeleza kuwa lakabu ni jina linalopewa mtu katika jamii ambalo hueleza kwa ujumla maumbile na tabia za mtu huyu. Kutokana na lakabu ni rahisi kuelewa ni tabia zipi zinazokubaliwa katika jamii na pia hudhihirisha ni maumbile yapi yanayoshabikiwa katika jamii fulani. Kwa kurejelea wazo linalowasiliswa na lakabu, Candrea (2001) anaainisha lakabu katika makundi mawili: Lakabu za kipekee na zile za kijumla. Katika kundi la lakabu za kipekee kuna lakabu mbalimbali kama vile:

(a) Lakabu zinazoonyesha maumbile ya mtu (umri, sura ya kutisha)

(b) Lakabu zinazoonyesha maadili ya mtu hasa dosari (ujinga, uchawi, ulevi, ujeuri, uchoyo, uchafu majivuno, ugomvi, kiburi, ulafi, ufidadi, unafiki, uoga, ukafiri, uvivu).

(c) Lakabu zinazohusu hadhi ya mtu katika jamii (umaskini, kazi duni au zenye kuleta hizaya)

Lakabu za kijumla ni zile zinazotumika katika mataifa mbalimbali kwa mfano lakabu Baba wa taifa kumrejelea kiongozi au raisi wa nchi.

2.3 Mbinu mbalimbali za kubuni lakabu

Lakabu hubuniwa kwa kurejelea jinsi jina la mtu lilivyo au kwa kurejelea sifa mbalimbali kumhusu mtu huyu. Mathalani, lakabu inaweza kurejelea cheo cha mtu. Cheo huhusu kazi anazofanya mtu au wadhifa wake katika jamii. Maumbile ya mtu kama vile: kimo chake, uzito alionao, nywele zake, sura yake, mkono anaotumia kufanya kazi na pia namna macho ya mtu yanavyoonekana inaweza kutumika kuzua jina la lakabu.

Felecan (2009) anapambanua lakabu kwa kurejelea muundo wake. Anaeleza kuwa kuna lakabu ya neno moja, lakabu ya kirai, lakabu ya sentensi na lakabu za methali. Anaeleza kuwa lakabu ni ubunifu unaofuatia urekebishaji wa muundo wa ndani wa fonimu ya neno linalotumika kumrejelea mtu. Felecan (2012) anadai kuwa kwa kurejelea semantiki tunaweza kuwa na lakabu changanuzi, lakabu linganifu na lakabu hekaya.

Lakabu changanuzi hudhihirisha msimamo wastani kuhusu anayepewa jina la lakabu. Baadhi ya lakabu hizi hurejelea maumbile kama vile mtu anaweza kuwa mfupi sana au mrefu sana ama pengine akawa na viungo vya mwili ambavyo ni vikubwa zaidi ya kawaida au vidogo zaidi ya matarajiwa; yaani kuna dosari katika maumbile. Hapa viambishi awali na tamati au vivumishi vya sifa hutumika. Mifano mingine ya lakabu changanuzi ni kama vile lakabu zinazoonyesha rangi (kama ngozi ni nyeupe au nyeusi) dosari ya macho, pua, mdomo, nywele, ngozi na lakabu zinazoonyesha uraibu na mahusiano mengine ya kiisimu.

Lakabu liganifu hutafsiri wasifu wa jumla unaomilikiwa na mtumizi wa lakabu. Kuna lakabu zinazotungwa kwa kutumia vivumishi vya sifa na lakabu zinazotumia istitari. Lakabu za hekaya hueleza matukio muhimu katika maisha ya mpokeaji wa jina la lakabu. Kuna pia lakabu zinazotokana na majina asilia ya mtu, mahali mtu alipozaliwa au lakabu zinazotokana na kazi anazofanya mtu. Lakabu huweza kuzuka kupitia ufupishaji au ubadilishaji wa jina. Jina halisi la mtu likiwa refu linaweza kufupishwa. Mathalani kutokana na jina Margret tunaweza kuwa na lakabu *Grata*. Herufi za mwanzo za majina ya watu zinaweza kutumika kama lakabu. Kwa mfano, jina Felix Rajabu huwa *F. R.* Baadhi ya silabi katika jina halisi la mtu zinapodondoshwa basi tunaweza kupata jina la lakabu, ni kutokana na mchakato huu ambao jina Leonard hufupiswa na kuwa lakabu *Len*. Pia sehemu mbalimbali za jina zinaweza kutegwa na kuwa lakabu. Kwa mfano, kutokana na sehemu ya mbele ya jina Christopher tunapata lakabu *Chris*. Kutokana na sehemu ya mwisho ya jina Andrew tunaweza kupata lakabu *Dew*. Kutokana na sehemu ya kati ya jina Elizabeth tunaweza kupata lakabu *Liz*.

Utohozi ni mbinu nyingine inayotumika katika uundaji wa lakabu. Kutohoa ni usawazishaji wa maneno kutoka lugha nyingine ambayo huwa matamshi au huandikwa kwa namna inayofanana na ile ya lugha chanzo kwa kufuata sarufi ya lugha lengwa. Katika utafiti huu wa sasa lakabu za wachezaji kandanda za lugha ya Ekegusii ziliainishwa kwa kurejelea muktadha wa kijamii na pia kwa kurejelea mtazamo wa kiisimu ili kutathmini namna zilivyobuniwa.

2.4 Matumizi ya lakabu katika jamii

Jina ni muhimu sana katika jamii. Jina humpa mtu hadhi ya juu au ya chini katika jamii. Ibuken (2009) anaeleza namna wanafunzi wa vyuo vikuu hujibadili majina na kujipa majina ya lakabu wanayofikiria kuwa yatawavumisha zaidi na kuwapa hadhi katika jamii. Baadhi ya lakabu hutumika kisiri na huweza tu kutajwa hadharani wakati wa mzozo au kwa nia ya kumkasirisha anayerejelewa. Majina haya huwa ni sitiari na huweza kusifia mtu au kumkashifu. Kwa mujibu wa Tunner (1997) mara nyingi lakabu hutumika kumtambulisha mtu au kudhihirisha kutoridhishwa na msimamo au tabia za mtu fulani au hutumika kukejeli uhasama. Matumizi ya lakabu huathiri maisha ya mtumizi wa lakabu kulingana na mahusiano ya kijamii yanayomhusu mtu huyu. Utafiti huu wa sasa uliangalia athari za kutumia lakabu katika mchakato wa kucheza kandanda ili kubaini iwapo majina haya ya lakabu yana umuhimu wowote katika kubadili mkondo wa mchezo huu wa kandanda yanapotumiwa na wachezaji au mashabiki wa mpira. Pia uliangalia iwapo lakabu hizi zinapotumika humtambulisha mchezaji au kuonyesha kuridhika au kutoridhika na msimamo wa mashabiki au tabia za wachezaji fulani au hutumika kukejeli namna wachezaji fulani wanavyocheza mpira.

Phafoli (2009) ni mtafiti aliyekusudia kudhihirisha kinachowachochea wasanii wa kabila la Bosotho kutumia majina ya lakabu katika maonyesho yao na hata kutumia lakabu zizi hizi kwenye kaseti na hata kanda zao. Katika utafiti Phafoli (2009) alidhihirisha kuwa majina haya ya lakabu za wasanii yalikuwa na

athari chanya kwa wasanii na umma. Kwa upande wa wasanii, lakabu ziliwazolea sifa nyingi na kuwafanya kujulikana kote na hivyo kuwaongezea kipato maradufu. Majina ya lakabu yaliwasaidia wasanii hawa kukuza nyimbo zao na pia kupiga jeki kiwango cha uchumi wao kwani kuliwaongezea soko pamoja na idadi ya mashabiki. Hivyo basi kwa upande wa biashara inadhihirika kuwa lakabu hukuza biashara. Kwa upande wa mashabiki kuna ile hali ya mwambata kwa msanii kwa sababu wasanii hawa huwa ni wananchi wanaoimba na kuvurumisha kijiji au nchi yao. Fahari yao kuu hujikita katika ufanisi wa msanii na kiwango cha ubora wa mziki anaoubuni.

Wainaina (2013) alionyesha pia namna majina ya lakabu yalivyowasaidia wanasiasa wa mkoa wa kati kushinda katika siasa. Anatoa mifano mitatu ya wanasiasa ambao majina ya lakabu yaliwasaidia sana kufaulu katika vinyang'anyiro mbalimbali vya kisiasa katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa elfu mbili na kumi na tatu katika mkoa wa Kati. Wanasiasa hawa waliamua kutumia majina ya lakabu waliyokuwa wamepewa na wananchi kutokana na majukumu mbalimbali waliyokuwa wametekeleza katika jamii. James Mathenge Simion, kwa mujibu wa Wainaina (2013) ni mwanasiasa ambaye alifaidika sana katika siasa kwa sababu ya kutumia jina lake la lakabu ambalo ni *Kanini Kega*. Jina hili la lakabu lilimsaidia kuwapiku wapinzani wenzake kwa kura elfu arobaini na nne. Mmoja wa wapigaji kura kwa majina Nemeysus Warugongo alieleza kuwa jina hilo la lakabu la mbunge wao lilikuwa linafahamika zaidi kijijini kuliko majina halisi ya mbunge huyu.

Francis mwangi kutoka Muranga alitumia jina lake la lakabu lililowachochea watu kumpigia kura nyingi hadi kuwashinda vigogo wa siasa waliokuwa wamepigiwa upatu wa kushida kinyang'anyiro hicho cha ugavana. Gavana Francis Mwangi ambaye alikuwa zamani mkurugenzi wa kampuni ya kitaifa ya kutengeneza maziwa, aliamua kutumia jina lake la lakabu la *Mwangi wa Iria* ili kumtofautisha na mpinzani wake mkuu ambaye alitwa daktari Mwangi. Mmoja wa wapiga kura kwa jina Joseph Kibe alieleza kuwa japo hakumfahamu Bwana Mwangi Francis, jina lake la lakabu lilimkumbusha namna alivyosaidia kufufua

kampuni hii ya kitaifa ya kutengeneza maziwa iliyokuwa imefilisishwa na ufasidi hivyo wakashawishika kumpigia kura na akaweza kupata kura elfu mia tatu thelathini na tano, mia mbili themanini huku mpinzani wake akipata kura elfu arobaini na tatu mia moja na tatu.

Kimani Paul ni mwanasiasa aliyefaidika sana kwa kutumia jina lake la lakabu katika siasa. Jina hili la lakabu lilimpa umaarufu na kumwezesha kumpiku mpinzani wake mkuu bilionea Bwana Githunguri aliyekuwa ametumia shilingi bilioni mbili katika kampeni zake. Akina mama wengi walimpigia kura walipoona jina lake Paul la lakabu katika karatasi ya kupigia kura. Jina *Matangi* walikuwa wamempa Bwana Kimani kwa sababu ya juhudi zake za kuwapa magari ya maji hivyo kumwezesha kupata kura elfu mia tano sitini na sita, mia tano tisini na tatu huku wapinzani wake wengine wote kwa pamoja wakipata chini ya kura elfu mia moja.

Wanasiasa wengine waliohalalisha majina yao ya lakabu kuwa majina yao halali ni kama vile Mheshimiwa Fedinard Waititu, *Baba yao* ambaye alikuwa gavana wa kaunti ya Kiambu na Mheshimiwa Mbuvi, *Sonko* ambaye alikuwa gavana wa kaunti ya Nairobi. Kazi hii ya Wainaina (2013) ni dhahirisho kuwa majina ya lakabu huwa na athari yanapotumiwa ikilinganishwa na majina halisi ya mtu hivyo kuchochea utafiti huu wa sasa uliolenga kubaini umuhimu wa matumizi ya lakabu katika mchakato wa mchezo wa kandanda.

Felecan (2009) anasisitiza kuwa mara nyingi lakabu hutokana na tabia hasi alizo nazo mtu. Kwa maoni yake lakabu ni majina yanayopewa mtu kwa lengo la kutumika kutambua wasifu wa mtu. Candrea (2001) anafafanua lakabu kama maneno yanayotumiwa na watu kukashifu tabia mbovu za mtu. Utafiti wake Candrea ulionyesha kuwa ni wasifu hasi pekee unaostahili kubuniwa lakabu mwafaka. Hata hivyo, hatuwezi kujifunga katika matumizi ya lakabu kuwa utambuzi wa wasifu pekee hivyo basi utafiti huu wa uhakiki wa kisemantiki wa lakabu za EkeGusii za wachezaji wa mpira wa kandanda yalikusudia kuainisha matumizi yote ya majina ya lakabu yakiwemo namna yanavyohalalisha tabia za mtu na inavyokashifu wasifu hasi unaotokana na maumbile ya mtu na hata matendo ya mtu.

Mashiri (2004) anaeleza kuwa majina ya lakabu huwa na matumizi yafuatayo: kubembeleza, kuwatenga watu kimaksudi, kuwashinikiza watu fulani kutenda jambo fulani katika jamii, kuwakashifu au kuwadunisha watu, kuonyesha urafiki wa karibu na pia kuwasifu watu fulani. Felecan (2009) anajikita katika utafiti wa mawasiliano ya lakabu na kupambanua lakabu hizi katika makundi mbalimbali kutokana na thamani yake ya kisemantiki. Pia, anaonyesha namna baadhi ya lakabu zilivyochimbuka katika jamii ya Warumi na namna huathiri mahusiano na maisha ya wanaopewa lakabu hizi. Kazi hii ilikuwa dira katika kuchunguza matumizi ya lakabu za EkeGusii pia utafiti huu wa sasa unashughulikia dhana zilizotumika kutambua maana ya lakabu zilizotumika masuala ambayo hayakushughulikiwa katika utafiti wake Felcan (2009).

SURA YA TATU

MUUNDO NA UTARATIBU WA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Ukusanyaji data ni shughuli muhimu sana katika utafiti wowote ule. Sura hii inashughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, washiriki wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ala na mbinu za utafiti na maadili ya utafiti.

3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo kwa sababu data iliyokusanywa ilikuwa ya kiuthamano, hivyo basi ilihitaji kufafanuliwa kupitia maelezo ya kina. Asilimia kubwa ya tafiti zinazohusu lugha, isimu, na fasihi ni za kimaelezo. Aina hii ya utafiti huwa haina mambo mengi changamano, hii ni kwa sababu utafiti hulenga mambo yalivyo pasipo kubadili vidadili (Buliba, Gwachi & Matinde, 2014). Suala la lakabu ni suala la kijamii linalohitaji masimuli ya mambo kuhusu wasifu wa mtu binafsi, makundi na hali mbalimbali hivyo basi kushadidi matumizi ya muundo wa utafiti wa kimaelezo.

3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Kenyena lililomo katika jimbo la Kisii. Wengi wa wakazi wa Kenyena huzungumza lugha asili ya EkeGusii. EkeGusii huzungumzwa na watu wa kabila la AbaGusii ambao ni wabantu wanaoishi nchini Kenya hasa katika majimbo ya Kisii na Nyamira. Kwa mujibu wa Nurse na Philipson (1980), EkeGusii kinahusiana na Kikuria, lugha inayozungumzwa Kenya na Ngurimi

na Zanaki zote zinazozungumzwa nchini Tanzania. Maho (2008) katika uchambuzi wake anaiita lugha ya Gusii. Ripoti ya sensa ya mwaka wa elfu mbili na tisa ilionyesha kuwa lugha ya EkeGusii ilikuwa na wazungumzaji, milioni mbili elfu mia mbili na tano, mia sita sitini na sita. Ripoti ya sensa ya mwaka wa elfu mbili na kumi na tisa ilionyesha kuwa jimbo hili dogo la Kenyenyema lina wakazi wapatao elfu mia moja na thelathini na moja mia saba arobaini.

Utafiti ulifanyika katika wodi zote nne za Kenyenyema (Boochi Borabu, Majoge Borabu, Majoge masaba na Magenche). Eneo hili la Kenyenyema lilichaguliwa kwa sababu kuna timu za kandanda sitini na moja ambazo zimesajiliwa na chama cha kitaifa cha mchezo wa kandanda na kuruhusiwa kushiriki michuano ya mpira katika nyuga mbalimbali za jimbo hili ndogo la Kenyenyema. Wengi wa wakazi wa Jimbo hili dogo la Kenyenyema ni mashabiki wa mchezo wa kandanda na wao hupenda sana kutumia lakabu waziwazi katika michakato ya mchezo wa kandanda. Kenyenyema ni jimbo ambalo liko mbali sana na mji wa Kisii hivyo wakazi wa mji wa kenyenyema wanazungumza lugha asilia ya EkeGusii ambayo haijaathiriwa na utamaduni wa kimagharibi. Hivyo basi ilikuwa rahisi kukusanya data nyingi (Lakabu) asilia za EkeGusii zilizotumika katika utafiti huu.

3.4 Washiriki wa utafiti

Utafiti wowote unaohusu lugha unastahili kulenga washiriki ambao sio wachanga sana na pia wanastahili kuwa wazugumzaji asilia wa lugha inayofanyiwa utafiti na wasio na matatizo ya matamshi kama anavyopendekeza Bower (2008). Utafiti huu uliwalenga wachezaji na mashabiki wa mpira wa kandanda waliotimiza masharti haya ya Bower. Lakabu za wachezaji mia mbili arobaini na mbili walio na umri kati ya miaka kumi na minane hadi thelathini na tano kutoka katika wodi zote nne za Kenyenyema ndizo zilizofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu.

3.5 Uteuzi wa sampuli

Utafiti huu uliegemea uteuzi wa sampuli kusimamia washiriki wote kwani sio rahisi kufanya utafiti kwa kila mtu. Johnstone (2008) anapendekeza kuwa sampuli nzuri inastahili kuwa na watafitiwa wengi waliochaguliwa bila kuwa na mpangilio maalum. Kati ya wachezaji wa timu sitini na moja zilizosajiliwa na wizara ya maswala ya vijana pamoja na michezo, lakabu za wachezaji kutoka kwa timu kumi na tisa ndizo zilizochunguzwa. Idadi hii inaoana na kiwango cha sampuli cha asilimia thelathini cha idadi jumulifu inayopendekezwa na Kothari (2004) kuwa na uwezo wa kuzalisha data yenye tabia wakilishi. Timu hizi ziliteuliwa bila mpangilio maalum kwa sababu timu hizi ni maarufu zaidi na huwa na mashabiki wengi kutoka vijiji vyote vya wodi zote nne za jimbo dogo la Kenyenia. Pia timu hizi huwa na michuano kila mwisho wa juma hivyo ilikuwa rahisi kupata majina mengi ya lakabu yaliyotumika katika utafiti huu.

3.6 Ala na mbinu za kukusanya data

Ala ni vifaa vilivyotumika katika utafiti. Utafiti huu ulitumia vifaa vitatu navyo ni; kinasa sauti, daftari na kalamu. Kinasa sauti kilitumika kunasa mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa ambao walikuwa ni wachezaji na mashabiki sugu wa mchezo wa kandanda kuhusiana na majina ya lakabu. Daftari lilitumika kuandika hoja zilizokusanywa katika utafiti. Kalamu ilitumika kujazia hoja kwenye daftari. Mbinu zilizotumika katika utafiti zilikuwa ni: kutazama michuano, kushiriki kwa kusikia na kunakili lakabu mbalimbali na mahojiano ya moja kwa moja ambayo yaliongozwa na maswali mahususi yaliyotokana na madhumuni ya utafiti.

3.6.1 Mahojiano

Mahojiano ni mazungumzo rasmi ya ana kwa ana baina ya mtafiti na mhojiwa au wahojiwa kwa minajili ya kuibua habari maalum inayohitajika katika utafiti (Buliba, Gwachi & Matinde, 2014). Henn, Wemsten na Foard (2006) wanaeleza kuwa mahojiano huwa muhimu hasa mtafiti anapohitaji kujihusisha moja kwa

moja na utafiti. Ili kufanikisha mbinu hii, mtafiti alitayarisha maswali ya mahojiano huku akiongozwa na mahiri wa somo hili. Maswali haya yalikuwa muhimu kwa sababu yalimwongoza mtafiti kuweza kupata data aliyohitaji bila kusahau mambo muhimu. Maswali haya ya utafiti yalimsaidia mtafiti kijifunga kwenye mada lengwa.

Mtafiti alijitahidi pia kujenga uhusiano mzuri na mhojiwa. Iwapo asingekuwa na uhusiano mzuri basi kuna uwezekano mhojiwa angekataa kuzumgumza. Mtafiti alitumia ishara mwafaka na pia lugha mwafaka alipotangamana na wahojiwa. Katika utafiti huu lugha mwafaka, ilikuwa ni lugha ya EkeGusii. Maswali yaliyochaguliwa na mtafiti katika utafiti huu wa majina ya lakabu yalikuwa maswali wazi ili kumpa mhojiwa nafasi nzuri ya kujieleza vilivyo. Maswali haya yaliulizwa kwa mfuatano wa kimantiki na mtafiti akahakikisha kuwa mhojiwa alielewa swali kabla ya kumpa muda ili ajieleze. Mtafiti alitumia kanda za kunasia sauti na pia aliweza kunakili mahojiano haya katika maandishi. Tafiti zingine hasa zilizohusu mapitio ya maandishi zilifanyiwa maktabani kutokana na kazi teule, majarida, magazeti, tasnifu na kwa mtandao. Data zote ziliyokusanywa ambazo ni lakabu zilidhibitishwa na wataalamu watatu wa lugha ya EkeGusii ambao walichaguliwa kimaksudi kutokana na umri wao mkongwe na weledi wao lugha na tamaduni za AbaGusii.

3.6 Maadili ya kiutafiti

Utafiti huu ulirejelea mapendekezo yake Bower (2008) kuhusiana na masuala ya maadili. Anasema kuwa katika utafiti wowote unaohusu lugha, mfumo wa maadili ni sharti uzingatiwe nao unahusu yafuatayo: kuwatambua watakaoshiriki katika utafiti, kuwaomba idhini watakaoshiriki katika utafiti, kuzuia kuwadhuru waasiliwa, kuomba ruhusa kufanyia utafiti lugha fulani na kuwashirikisha wale wanatafiti. Mtafiti aliheshimu kazi za watafiti wengine na pia aliponakili kazi za wengine alionyesha kazi hiyo hasa ilikuwa ya nani kama walivyopendekeza (Chelliah na Reuse 2011).

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UHAKIKI WA DATA

4.1 Utangulizi

Baada ya kukusanya data mtafiti aliipanga data yake vizuri na kuiwasilisha kwa utaratibu uliowazi. Dey (1993) anaeleza kuwa uwasilishaji wa data unahusu kupanga data katika vipengele vidogo vidogo muhimu vitakavyosaidia katika ufasiri wa data hiyo. Upangaji huu wa data ni muhimu sana katika utafiti. Hatua ya kwanza ya upangaji data ilikuwa mtafiti kuihariri data yake ili kujaza mapengo ambayo yalikuwepo,

kuyaondolea mbali yale ambayo hayakuhitajika na kuyarekebisha yale yaliyokuwa na mushkeli. Hatimaye mtafiti aliyafasiri matokeo ya uchanganuzi ili kufikia maamuzi.

Ukusanyaji na uwasilishaji wa data katika utafiti huu uliongozwa na nadharia ya semantiki ya fremu. Hii ni kwa sababu nadharia ni muhimu sana katika utafiti wowote ule wa kitaalamu. Abrahamson (1983) anasisitiza kuwa hamna utafiti unaoweza kukamilika bila kuonyesha nafasi iliyochukuliwa na nadharia. Data ambazo ni lakabu za EkeGusii zilikusanywa, zikatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili bila kupoteza maana iliyokusudiwa. Data hizi zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya semantiki ya fremu. Hatua ya kwanza ya uchanganuzi ilikuwa kutambua lakabu na kuziweka lakabu hizi katika makundi mbalimbali ili kurahisisha ufafanuzi wa kisemantiki wa lakabu hizi kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya fremu. Hivyo basi kila lakabu katika utafiti huu ilitambuliwa na kuainishwa kisha kuwasiliswa ifuatavyo: Lakabu katika matini ya lugha ya EkeGusii kutumia nambari za kiarabu, maelezo ya kiisimu ya lakabu yanayojumuisha maana tambuzi (halisi) au maana ya kijuujuu, maana ashirifu au maana batini inayodokeza maana ya ndani ya lakabu pamoja na asili (namna lakabu huchimbuka au chimbuko la lakabu). Hatua ya pili ilikuwa kubainisha mbinu mbalimbali zilizotumika kubunia lakabu hizi. Kisha hatua ya mwisho ya uchanganuzi ilikuwa kupambanua matumizi ya lakabu katika mchakato wa kucheza kandanda. Sura hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kwa mujibu wa madhumini makuu ya utafiti nayo ni: kubainisha maana ya lakabu za EkeGusii zinazotumiwa na wachezaji kandanda, kufafanua mbinu mbalimbali za lugha zinazotumiwa kubuni lakabu za lugha ya EkeGusii za wachezaji kandanda na Kupambanua matumizi ya lakabu za EkeGusii katika mchakato wa kucheza kandanda.

4.2 Maana ya lakabu teule za EkeGusii za wachezaji kandanda

Kulingana na utafiti huu lakabu huweza kuwa na maana nyingi tofautitofauti kutegemea nyakati pamoja na miktadha mbalimbali. Dhamira ya matumizi ya lakabu kulingana na mtoaaji wa lakabu hiyo pia huongezea

maana ya lakabu kwani hueleza hadhithi kuhusu anayerejelewa na lakabu hiyo au ethinografia ya mrejelewa. Maana katika lakabu sawa na ilivyo katika methali hushughulikiwa katika viwango viwili navyo ni: maana ya wazi (tambuzi) na maana batini (ashirifu). Maana ya wazi katika utafiti huu ni karibu sawa na maana halisi inayoibuka baada ya uchanganuzi wa kiisimu. Maana hii inaweza kurejelewa kama maana ya lakabu kulingana na kamusi kwa sababu maana hii inatokana na thamani ya kisemantiki ya vipengele vya isimu vinavyotumika katika lakabu. Hata hivyo maana ashirifu hupatikana tu baada ya kufanya uchanganuzi wa usuli wa lakabu hizi. Hivyo basi maana ashirifu ndiyo inayorejelewa kama maana halisi katika utafiti huu.

Ili kubainisha maana ya lakabu, utafiti huu ulitumia nadharia ya fremu inayoeleza namna tunavyotambua maana ya majina kutokana na elimu aliyonayo mtu kupitia matumizi ya dhana zinazohusiana. Elimu ni habari azijuazo mtu kuhusu majina haya ya lakabu. Kulingana na waasisi wa nadharia hii, dhana ya neno inaweza kueleweka kwa kurejelea vielelezo vilivyomo akilini mwa mtu ambavyo vinatokana na uzoefu wa siku nyingi. Filmore (1985) anaeleza kwamba nadharia ya semantiki ya fremu hujaribu kufafanua maana kwa kuhusisha neno hili na usuli wake. Nadharia hii inashikilia kuwa maana huoana na mandhari hivyo basi maana inaweza kudhihirika kutegemea usuli au mandhari. Kwa kurejelea mihimili ya nadharia ya kisemantiki ya fremu pamoja na dhana za kisemantiki; maana wazi na maana halisi ya lakabu za wachezaji kandanda za EkeGusii, tunaweza kupata fremu muhimu zinazosaidia kueleza maana kwa njia sahili. Utafiti huu uliainisha lakabu katika makundi yafuatayo:

Kikundi cha lakabu	Mifano
Lakabu zinazoonyesha maumbile na rangi	<i>Embiro, Omorambeke, Rigento, Matacho, Gekuba, Rikongo, Mura, Matiende, Matingi, Matogoro, Ontogoro, Egecheru, Serenti,</i>

	<i>Manungu, Motambesi, Bitege, Omongina, Ringina, Rigege Magoro, Mobere, Kebue, Nyamotwe, Nyamoto.</i>
Lakabu zinazowasilisha sifa mbalimbali	<i>Ribambo Simbiri, Ritukutuku, Nyandamwamu, Mabera, Suru, Ogosa, Oseko, Mogiti, Okirimiti, Matiebo, Okemanyi, Otwoma, Enterere, Ochusi, Nyamunsi, Echabu Omochuri Richuma, Enkongo, Rikunyati, Enchome, Egiata, Omong'iti</i>
Lakabu za wanyama wa mwituni, wa kufugwa na wa majini	<i>Enchogu, Egesusu/Agasusu Ebunda, Ebeche Eng'iti, Enchoka, Esimba, Gechure/Egechure, Enswe, Enkonye, Egesimba, Endo, Emamba, Egesia, Embori, Egioto, Echui, Ribumburi, Ekenyamato,</i>
Lakabu za ndege na wadudu	<i>Embogo, Egesase, Enguncho, Enchoke, Ensona Ensanako, Ribundu, Egechibi, Ekenyinyi, Ritimbo, Egesam, Ekiaramba, Egechuchuti</i>
Lakabu za mimea	<i>Ekenagwa, Rikuneni, Emoti, Rinani, Egetuki, Masosa, Rikongiro, Enderema, Egechachuti.</i>
Lakabu zinazoonyesha matendo fulani	<i>Muntaari, Ontimbu, Ribotabota, Kwaruro,</i>

	<i>Ekerambauti, Egose, Embeo egousa, Boyia</i>
Lakabu zinazoonyesha vitu mbalimbali	<i>Ebunia, Ensara, Marionya, Egekenga, Oroteru, Egesigia Emesesi, Rigombi, Richwati, Rikorogoto, Enkoba, Ekebarabara, Omosungose, Egeuti, Egosia, Ekeboye, Risasi, Enguba, Rigena, Embombo, Eubi, Nyaanga, Ekebondo</i>
Lakabu za sehemu mbalimbali	<i>Riiko, Ritundubari, Ekenya, Ekeumbu, Etinga</i>

Jedwali linaloonyesha makundi mbalimbali ya lakabu

Uainishaji huu unaoana na ule uliofanywa naye Felecan (2000) ulioainisha dhana za kisemantiki za lakabu za Warumi katika kategoria zifuatazo: lakabu changanuzi, lakabu linganifu na lakabu hekaya. Lakabu changanuzi hudhihirisha msimamo wastani kuhusu anayepewa jina la lakabu. Baadhi ya lakabu hizi hurejelea maumbile kama vile mtu anaweza kuwa mfupi sana au mrefu sana ama pengine akawa na viugo

vya mwili ambavyo ni vikubwa zaidi ya kawaida au vidogo zaidi ya matarajiwa; yaani kuna dosari katika maumbile. Hapa viambishi awali na tamati au vivumishi vya sifa hutumika. Mifano mingine ya lakabu changanuzi ni kama vile lakabu zinazoonyesha rangi (kama ngozi ni nyupe au nyeusi) dosari ya macho, pua, mdomo, nywele, ngozi na lakabu zinazoonyesha uraibu na mahusiano mengine ya kiisimu.

Lakabu linganifu hutafsiri wasifu wa jumla unaomilikiwa na mtumizi wa lakabu. Kuna lakabu zinazotugwa kwa kutumia vivumishi vya sifa na lakabu zinazotumia istiari. Lakabu za hekaya hueleza matukio muhimu katika maisha ya mpokeaji wa jina la lakabu. Kuna pia lakabu zinazotokana na majina asilia ya mtu, mahali mtu alipozaliwa au lakabu zinazotokana na kazi anazofanya mtu pia kuna lakabu zinazotokana na sehemu anakoishi mtajwa. Lakabu zingine hutokana na majina ya familia. Maana na dhana za kisemantiki za lakabu zilizotajwa ziliweza kujadiliwa kwa undani kupitia mifano ifuatayo:

4.2.1. Lakabu za maumbile na rangi

Hizi ni lakabu zinazobandikwa mtu kwa sababu ya maumbile yake au rangi ya ngozi yake. Lakabu za maumbile ni lakabu ambazo asili yake ni maumbile ya mtumizi wa lakabu, anaweza kuwa mkubwa sana au mdogo sana. Viungo vya mwili vinaweza kuwa vikubwa au vikawa vidogo zaidi. Kwa ujumla kuwa na ulemavu wa aina fulani kunaweza kuwa chimbuko la kubatizwa lakabu kama inavyodhihiriswa na mifano ya lakabu zifuatazo:

4.2.1.1 Lakabu za maumbile

1. *Omorambeka*. Maana tambuzi ya lakabu hii ni barabara ndefu iliyonyooka. Hivyo basi kulingana na maarifa yaliyomo akilini mwa mtu kuhusu dhana hii (barabara) fremu zifuatazo zinajitokeza: urefu, wembamba na pia barabara huwa inaelekea mbali. Maana ashirifu ya lakabu hii inaibuka kutokana na kuzingatia fremu zinazohusiswa na neno barabara. Hivyo basi ni wazi kuwa lakabu

hii ni sitiari na inarejelea mchezaji mrefu zaidi kwa kimo na mwebamba. Kimo chake ndicho chimbuko la lakabu hii.

2. *Rigento* ni kitu kikubwa kisichokuwa na jina (maana tambuzi). Lakabu hii ni ya mchezaji mkubwa kimaumbile lakini asiyekuwa na umuhimu wowote uwajani. Ni lakabu ambayo mashabiki wa mpira walimbatiza mchezaji huyu kwa sababu ya mwili mkubwa ila hakuwa anautumia vyema kwa sababu hakuwa anajua kucheza mpira uwajani. Maana ashirifu ni jitu kubwa.
3. *Matacho* ni miguu mikubwa isiyo ya kawaida (maana tambuzi). Usuli wa lakabu hii ni nyayo za ndovu waliokuwa wanapitia katika kaunti hii ya Kenyenyema kutoka mbuga la wanyama la Maasai mara kuelekea Tanzania. Taswira hii ya miguu ya ndovu ndiyo inayoelekeza kutambua maana ashirifu ya Lakabu hii. Huyu ni mchezaji mwenye miguu mikubwa sana uwajani ambaye ni tegemeo la timu yake. Kila mara anapokuwa uwanjani anawafanya wachezaji wengine kubabaika. Mpira humpiti uwanjani.
4. *Gekuba*. Maana tambuzi ya lakabu hii ni sehemu ya mbele ya mwili kati ya tumbo na shingo ambayo kuna mapafu na moyo ndani yake; kifua. Maana ashirifu ni mchezaji mwenye kifua kikubwa. Mchezaji huyu alikuwa anatumia kifua chake kwa ufasaha kutuliza mpira hivyo kuwachochea mashabiki wake kumbandika lakabu hii. Ni mchezaji mkakamavu atumiaye nguvu nyingi uwanjani na kuisaidia timu yake kufunga mabao mengi.
5. *'Rikongo'* ni ng'ombe mzee (maana tambuzi). Ng'ombe ni mnyama afugwaye lakini mdogo anayefanana na nyati ambaye anafaida kadha kama vile nyama, maziwa na ngozi. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji mkongwe uwanjani ambaye alikuwa na tajriba ya kucheza mpira kwa miaka mingi. Licha ya kukonga huyu ni mchezaji aliyekuwa na manufaa kwa sababu ya tajriba yake, hata hivyo ni mchezaji asiyekuwa na kasi na wakati mwingine kwa sababu ya umri wake mkogwe

aliweza kusababisha hasara kama vile kushidwa kuudhibiti mpira. Fremu zilizojitokeza zinaelekeza maana ashirifu ya lakabu ambayo ni mchezaji mkongwe. Pia ni lakabu ambayo mashabiki walimpa mchezaji anayejikokota uwajani ili kumkejeli.

6. *Mura*. Usuli wa lakabu hii ni kufipisha jina ‘*momura*’ linalomaanisha mvulana ili liwe *mura* linalomaanisha kuficha kitu fulani. ‘*Momura*’ ni mvulana aliyeenda jandoni. Katika jamii ya AbaGusii jando ni muhimu sana kwa sababu wakati wa jando ndipo mvulana huelezewa siri zote za jamii naye huhitajika kuzihifadhi. Lakabu hii ‘ilibatizwa’ mchezaji shupavu na mwenye nguvu. Mchezaji huyu aliposhika mpira hakuna mchezaji mwingine aliyeweza kuuona au kuuguza huo mpira.
7. ‘*Matiende*’ ni miguu iliyovimba kutokana na kuambukizwa ugonjwa wa matende (maana tambuzi). Maana ashirifu ni miguu mikubwa kama ya ndovu. Kwa kawaida ndovu huwa ni mnyama mkubwa mwenye miguu mikubwa hivyo basi maana ashirifu ya lakabu hii ni mguu mkubwa kama ya ndovu. Hii ni lakabu iliyorejelea mchezaji ambaye miguu yake ni mikubwa na yenye nguvu kama ya ndovu.
8. ‘*Matingi*’. Maana tambuzi ni miguu mifupi nayo maana ashirifu ni aliye na miguu minene iliyo thabiti. Lakabu hii ilitokana na maumbile ya mchezaji aliye na miguu minene iliyoimara.
9. ‘*Matogoro*’ ni macho makubwa (maana tambuzi) Huyu ni mchezaji ambaye ana macho makubwa kuliko yale ya kawaida. Mashabiki walimbatiza lakabu hii kwa sababu alipokondoa macho haya yake yalistusha kwa sababu ya ukubwa wake hivyo kumfanya kuwaogofya mashabiki na hata wachezaji wengine. Dhana hii ya kuwa na macho makubwa inaelekeza ufumbuzi wa maana ashirifu nayo ni kufugua macho kwa nia ya kushtua au kukasirisha.

10. *'Manungu'* ni mgogo uliolemaa (maana tambuzi). Lakabu hii ilichipuka kutokana na jina la EkeGusii *'Omonungu'* kumaanisha lemaza au atilisha sehemu fulani ya mwili. Usuli wake ni maumbile ya mchezaji huyu baada ya kufanya mazoezi sana misuli inapanuka hivyo anapotembea mgogo wake unaonekana kupinda. Pia ilitokana na nomino *'Enungu'* iliyomaanisha rungu, hivyo unapomtazama mchezaji huyu ni kana kwamba amebeba rungu mgongoni. Hivyo basi maana ashirifu ni mchezaji anayecheza mpira uwanjani mgogo ukiwa umepinda. Hii ni ishara ya nguvu na bidii na ni mchezaji thabiti aliyecheza kwa muda mrefu uwanjani bila kuchoka. Lakabu hii ilitokana na ustahimilivu wake uwanjani.
11. *'Nyamioro'* ni kiungo cha mwili wa kiumbe, chenye tundu, kilicho juu ya mdomo kinachomwezesha kuvuta pumzi na kunusia; pua kubwa (maana tambuzi). Lakabu hii ilibandikwa mmiliki na mashabiki kwa sababu ya kuwa na mwili mdogo lakini pua kubwa isiyokuwa ya kawaida hivyo kumtabulisha hata akiwa mbali. Maana ashirifu ni mchezaji mwenye mwili mdogo na pua kubwa kuliko kawaida. Pia mchezaji huyu alikuwa ni mgomvi na alipenda kuzua ugomvi na vita uwanjani hivyo mashabiki wakampa lakabu hii ili kumkejeli.
12. *'Nyataya'* ni chombo kinachowashwa na kutoa mwanagaza ili kumulikia au kuangaza; taa (maana tambuzi). Maana ashirifu ni macho makubwa. Hii ilikuwa ni lakabu ya mchezaji mwenye macho makubwa zaidi ya wachezaji wenzake. Lakabu hii ilitumika kistiari kurejelea mchezaji shupavu ambaye mpira hukumpita uwanjani.
13. *'Nyamotwe'* ni kichwa (maana tambuzi). Lakabu hii ilikuwa ni ya mchezaji mwenye kichwa kikubwa ajabu kuliko mwili (*nyamotwe insiongo*). Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuugonga mpira kila mara kwa kutumia kichwa chake.

14. *'Motambesi'*. Maana tambuzi ni kimo cha mtu. Lakabu hii ilitokana na jina *'Obotambe'* inayomaanisha kipimo fulani kutoka upande mmoja hadi mwingine inaweza kuwa upande wa juu hadi chini au mbele hadi nyuma. Maana nyingine ilikuwa ni muda fulani uliotumika kufanya jambo fulani, tendo hili laweza kukamilika au isikamilike. Lakabu hii pia iliweza kutokana na kielezi *'Botambe'* lililomaanisha hali ya mazoea au kama kawaida. Pia ilimaanisha kulenga mbele na kufululiza bila kusimama. Kwa kuzingatia fremu hizi maana ashirifu ilidhihirika wazi kuwa hii ni lakabu ya mchezaji ambaye ni mrefu kwa kimo na pia ana uwezo wa kucheza mfululizo bila kuchoka ni mchezaji wa kutegemewa kwa sababu yeye ni mwenye bidii na ana mazoea ya kuupiga mpira ukaenda mbali sana uwanjani hii ni kwa sababu ya miguu yake mirefu.
15. *'Bitega'* ni miguu iliyopinda kwa nje kuanzia magotini; matungamavi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye miguu iliyopinda. Maumbile ya mchezaji huyu yaani kule kupinda kwa miguu yake ndicho kichocheo cha lakabu hii. Kulemaa kwa mchezaji huyu kulimsaidia kuweza kuudhibiti mpira uwajani. Huyu ni mchezaji mzuri sana.
16. *'Omongina'*. Maana tambuzi ni mama. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuzembea uwanjani. Uzembe huu wake ulimfanya kukejeliwa na mashabiki kwa kuitwa mama mkongwe. Mama ambaye amefikisha kikomo cha hedhi hivyo hatarajiwi kuzaa. Huyu mchezaji alikuwa ni mvivu na hakuwa na makali tena ya kuisaidia timu yake. Lakabu hii ilitatizwa mchezaji huyu na mashabiki kwa nia ya kumdhalilisha. Mchezaji mzembe (ashirifu).
17. *'Rigegu'* ni jino la mwisho ambalo hutumika kwa kutafunia chakula (tambuzi). Lakabu hii ni sitiari iliyotokana na matumizi ya jino hili ambalo hutumika kutafuna chakula. Mchezaji huyu ni nguzo ya timu yake ndiye kiungo tegemeo na msukumo wa timu yake kwani ana umahiri wa hali ya juu wa kucheza mpira.

18. *'Magoro'* ni kiungo cha mwili wa binadamu, mnyama au mdudu kinachomwezesha kusimama au kwenda; miguu (tambuzi). Lakabu hii ilitokana na ujuzi wa mchezaji huyu. Miguu yake iliukabili mpira kiasi kwamba yeye ndiye aliyekuwa nguzo ya timu yake, yeye ndiye aliyekuwa tegemeo hasa wakati wa kupasi mpira kwa wachezaji wenzake.
19. *'Mobere'* ni umbo lote la mnyama na binadamu kuanzia kichwani hadi miguuni (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na maumbile ya mchezaji huu. Ni mchezaji mwenye mwili mkubwa ilhali hana ujuzi wa kucheza mpira. Hasaidii timu yake kwa vyovyote vile. Yeye ni sawa na maiti-mwili tu bila uhai.
20. *'Embombo'* ni mpira (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na maumbile ya mchezaji huyu ambaye ana mwili mkubwa sana lakini ni mfupi, ukimtazama anaonekana kama mpira uliopulizwa. Maana ashirifu ni mchezaji mwenye mwili mkubwa.

4.2.1.2. Lakabu zinazohusu rangi

Hizi ni lakabu zilizobandikwa wachezaji kwa sababu ya rangi ya ngozi zao. Mtu anaweza kuwa mweusi sana au akawa mweupe sana kama inavyodhihirishwa na mifano ifuatayo:

21. *'Embiro'* ni Masizi (maana tambuzi). Masizi ni unga mweusi unaotokana na moshi wa moto ambao hupatikana kwenye sufuria au chungu. Lakabu hii ilitokana na rangi ya mchezaji huyu mbae ni nyeusi kama masizi. Maana ashirifu ni mchezaji mweusi sana.
22. *'Omosongo'*. Maana tambuzi ni mzungu. Jina mzungu linadokeza fremu zifuatazo: mtu mwenye asii ya ulaya, mbinu ya kujitoa katika matatizo, jambo la ajabu lisilo eleweka au mafunzo yatolewayo kwa vijana wa jando. Hivyo basi maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mweupe pepepe. Lakabu hii ilitokana na rangi ya mchezaji huyu ambaye ni mweupe. Pia lakabu hii ilitumika kistiari na mashabiki

waliotaka kumkejeli mchezaji mwenye ngozi nyeusi sana. Mchezaji mwenye maringo aliweza kujibandika lakabu hii kuonyesha jinsi alivyomstaarabu.

4.2.2.Lakabu zinazowasilisha sifa mbalimbali

23. '*Ribambo*'. Maana tambuzi ya lakabu hii ni mtu mwenye nguvu. AbaGusii ni jamii iliyokuwa ikipenda kushiriki katika mchezo wa mieleka na mshindi ndiye alikuwa anaitwa '*Rimbambo*'. Katika mchezo wa kandanda mara nyingi hii ilikuwa ni lakabu ya majigambo aliyojibandika mchezaji mwenyewe. Mashabiki pia waliweza kumpachika mchezaji yeyote aliyetokea kuwa na wasifu kama huu kwenye timu waliyoishabikia. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye nguvu na bidii. Huyu ni mchezaji aliyekuwa na nguvu na mwenye bidii uwanjani. Alipokuwa uwanjani, hakuna yeyote aliyeweza kumshinda au kumpokonya mpira.

24. '*Simbiri*' ni mtu mwenye mazoea ya kuchukua mali ya watu bila idhini yao, mtu anayeiba; mwizi, mwivu (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na ujuzi wa mchezaji huyu wa kunyakuwa mpira kutoka kwa wachezaji wa timu pinzani. Mchezaji huyu alikuwa na uwezo wa hali ya juu wa kuwapiga chenga wachezaji wengine na kuwanyanganya mpira. Maana ashirifu ni mchezaji matata hasa kwa kunyakua mpira kutoka kwa wapinzani (ashirifu).

25. '*Ritukutuku*' ni mlio unaotokana na kuwashwa kwa mtambo unaotoa nguvu zakuwezesha chombo kifanye kazi; injini (maana tambuzi). Asili ya lakabu hii ni kukerwa kwa mashabiki waliokasirishwa na mchezaji huyu ambaye alikuwa hakimbii kwa kasi uwajani hasa mashabiki hawa walipomtarajia akimbilie mpira ndipo apeana pasi kwa haraka au mchezaji huyu alipohitajika kukimbia ili kuokoa mpira usigonge wavu. Lakabu hii ni tanakali ya sauti iliyotolewa na injini ilipowashwa hivyo mchezaji huyu alifananishwa na sauti hiyo mbovu ya kukereketa sikio iliyotolewa na injini hii. Pia, kasi yake

ilifananishwa na muda mrefu uliotumika kutoa sauti hii ya ‘Tukutuku’. Maana ashirifu ni mchezaji ambaye hakimbii kwa kasi.

26. *‘Nyandamwamu’* ni tamaa ya kupata chakula, pesa, cheo, mali na mengineo zaidi ya vile unavyohitaji (tambuzi). Lakabu hii ilitokana na wasifu wa mchezaji huyu ambaye alikuwa mchoyo na pia alikuwa na tamaa ya kuucheza mpira peke yake bila kuwashirikisha wenzake. Huyu ni mchezaji mwenye ghadhabu na hasira kali. Mara nyingi yeye aligombana na kupigana na wachezaji wenzake uwajani, pia alikuwa na tabia ya kuwajeruhi wachezaji wa upinzani hasa alipoona ni wachezaji wazuri kusudi aonekane ni yeye aliyetamba pekee uwanjani. Lakabu hii ilipeanwa na mashabiki ambao walikuwa wamekerwa na tabia hii mbaya. Maana ashirifu ni mchezaji anayeshabikiwa sana kwa sababu ya tamaa yake ya kutaka kuudhibiti mpira peke yake bila kuwapokeza wengine.

27. *‘Mabera’* ni mtu mpole na mwenye huruma (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na wasifu wa mchezaji huyu wa kuwa na moyo wa huruma. Huyu ni mchezaji mpole na myenyekevu aliyefuata kanuni za mpira wa kandanda. Yeye alikuwa hana fujo na kila mara alikuwa tayari kuwasaidia wachezaji wengine waliopata matatizo uwanjani. Mara nyingi yeye alijitolea kutoa huduma ya kwanza kwa wachezaji wenza waliopata majeraha uwajani. Hivyo basi maana ashirifu ni mchezaji mpole na mwenye kuonyesha moyo wa imani kwa wachezaji wenzake hata kama ni wa timu pinzani (ashirifu).

28. *‘Suru’*. Maana ashirifu ya lakabu hii ni kupita bila kuzuiliwa popote. Lakabu hii ilitokana na neno la Kiswahili ‘haidhuru’ linalomaanisha pasipo na madhara, shida au athari kubwa; si kitu, hapana neno. Mashabiki wa kabumbu walimpachika lakabu hii mchezaji huyu kwa sababu ya weledi wake wa soka uliowapiku wachezaji wote uwanjani kiasi kwamba alipoushika mpira alikuwa na uwezo wa kuwachenga wachezaji wengine kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mechi bila kuzuiliwa na yeyote yule. Maana ashirifu ni mchezaji mweye ujuzi wa hali ya juu wa kuuchenga mpira.

29. '*Ogosa*' ni mchezaji mwenye kuogofya (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu ya majigambo huku akitoa cheche za maneno ya kuwashtua na kuwadhalilisha wapizani ili wasiweze kuwa na ujasiri wa kucheza vizuri. Maana ashirifu ni mchezaji mwenye kuwashtua wengine.

30. '*Oseko*' ni lakabu inayomaanisha kutoa kicheko (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na wasifu wa mchezaji huyu wa kupenda kucheka sana kila wakati alipokuwa uwanjani. Kucheka kwa mchezaji huyu kuliashiria kuwa yeye ni mtu wa furaha na tabasamu kila wakati hivyo maana ashirifu ni mchezaji mwenye kupenda kucheka.

31. '*Mogiti*' ni jina la mwanamke (maana tambuzi). Lakabu hii imefupishwa kutokana na neno '*Omogiti*' inayorejelea mtu mwenye kutengeneza ua. Lakabu hii ilimrejelea mlinzi shupavu ambaye alitegemewa sana kuhakikisha mpira hautikisi wavu. Kazi yake kuu ilikuwa ni kuzuia mpira kutoka sehemu ya upinzani isimfikie mlinda lako wa timu yao kwa kutengeneza 'ua' mbele ya mlinda lango.

32. '*Omong'iti*' ni hali ya kuwa bahili na kukataa kutoa kitu ulichonacho kwa manufaa ya watu wengine hata pale ambapo hukihitaji kitu hicho kamwe (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya uchoyo aliokuwa nao mchezaji huyu. Mchezaji huyu alipoushika mpira alikataa kata kata kuwapa pasi wenzake. Huyu ni mchezaji ambaye hatambui manufaa ya umoja na ushirikiano katika mchezo wa kandanda. Hivyo basi maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji anayejipenda sana uwanjani.

33. '*Okirimiti*' ni mtu asiyestarabika, mtu mwenye tabia ya kuwakera wengine (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huu kujipenda zaidi na kujiona bora kuwaliko wachezaji wengine uwanjani. Tabia hii ilimfanya kujitenga na wengine hivyo ni lakabu iliyotolewa na wachezaji wenza kwa sababu ya kukerwa na tabia hii mbovu ya mchezaji huyu, mchezaji anayejipenda sana uwanjani (ashirifu).

34. *'Matiebo'* ni blanketi baridi (maana tambuzi). Lakabu hii ilitolewa na wachezaji kumrejelea mchezaji mwenza ambaye alikuwa hana shauku wakati wa mechi. Tabia hii yake mabao na kusherekea ushindi. Kila mara alipopata pasi alipoteza nafasi ya kutingiza wavu. Lakabu hii pia ilimrejelea mchezaji mnene sana uwanjani kiasi kwamba hakuweza kuukimbilia mpira uwanjani. Huyu ni mchezaji aliyesambaratisha mipango ya wachezaji wengine. Maana ashirifu inayojitokeza ni kuwa, ni mchezaji asiye na shauku kwa lolote.

35. *'Otwoma'* ni kusukuma: kumfanya mtu asonge kwa kumsukua kutumia mikono yako au sehemu nyingine ya mwili (maana tambuzi) Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu ya kuwachokoza wachezaji wengine uwanjani hasa wale ya timu geni. Lakabu hii ilitokana na kitenzi 'twoma' yaani sukuma mtu au kitu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Huyu ni mchezaji mgovi aliyependa kuwachokoza wengine uwanjani kwa kuwasukuma ili wamwachie mpira. Maana ashirifu ni mchezaji mchokozi sana uwanjani.

36. *'Enterere'* ni lakabu inayomaanisha kitu telezi (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na kitenzi *'tereri'* iliyomaanisha kusepetuka mahali penye matope na hata kukaribia kuanguka. Pia ilimaanisha kusererereka au kuwa katika hali ya ulaini kwa mfano kamasi, ute, grisi au mafuta. Lakabu hii ilibatizwa mchezaji ambaye hangeweza kutegemewa uwajani kutokana na tabia yake ya kufanya makosa madogo madogo uwanjani na wakati mwingine kufanya makosa bila hata yeye kukusudia. Fremu hizi zinaelekeza utambuzi wa maana ashirifu nayo ni mchezaji mjanja.

37. *'Ochusi'* ni lakabu inayomaanisha ujuzi (maana tambuzi). Asili ya lakabu hii ni utohozi kutoka jina la Kiswahii 'ujuzi' linalomaanisha maarifa aliyonayo mtu katika kufanya kazi au jambo fulani. Huyu ni mchezaji ambaye alikuwa mwenye ufundi wa hali ya juu wa kusakata kambumbu uwajani, hasa huyu ndiye aliyekuwa mtaalamu wa soka, alipoingia uwanjani mashabiki walimshangilia kwa kuwa

walielewa kuwa lazima ataonyesha ujuzi wa hali ya juu uwajani na kufunga mabao mengi. Maana ashirifu ni mchezaji mwenye maarifa.

38. *'Okemanyi'* ni hali ya kujidai kujua kila kitu au kujua mno (maana tambuzi). Usuli wa lakabu hii ni hadithi ya mke wa Osoro ambaye alikuwa na tabia ya kujidai kuwa yeye alikuwa mjuaji wa kila jambo hata ingawa kuna mambo ambavyo hakuwa na maarifa kuyahusu. Mashabiki walimbadika lakabu hii mchezaji huyu kwa sababu alijifanya kuwa na ujuzi na maarifa ya kucheza soka kiasi kwamba alipuuzilia mbali ushauri wa kocha na kuishia kufanya makosa mengi uwanjani ambayo yangeweza kuepukika iwapo angelifuata ushauri. Hivyo basi maana ashirifu ni mchezaji mjuvi. Lakabu hii ilitumika kwa kusudi la kumkejeli mchezaji wa aina hii alipofanya makosa uwajani.

39. *'Nyamunsi'*. Maana tambuzi ni jina la mwanamke mnyamavu. *'Nyamunsi'* anaaminika kuwa mtu wa kwanza katika jamii ya AbaGusii kufuga na kuuza mnyama anayeitwa paka. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji ambaye alikuwa hapendi kuzungumza sana na alipendelea kukaa kimya hata pale ambapo alidhulumiwa na wachezaji wengine. Hii ni lakabu yenye toni ya jinsia ya kike kwa sababu mwanamme wa jamii ya AbaGusii hatarajiwi kunyamaza na kuvumilia dhuluma kutoka kwa yeyote. Hivyo basi lakabu hii itumika kumdhihaki mchezaji wa aina hii. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mpole na mnyamavu.

40. *'Richuma'* ni kibaraka (maana tambuzi). Usuli wa lakabu hii ni utohozi wa neno la Kiswahili chuma linalomaanisha jabali la mtu yaani mtu mwenye nguvu nyingi. Ni lakabu iliyotumiwa na wanakijiji kuwarejelea mamluki waliokuwa wamekodishwa mwaka wa elfu mbili na tatu wakati wa mazishi ya aliyekuwa mbuga wa Mugirango kusini mheshimiwa hayati Enock Nyankieya Magara, kuwasaka waliokuwa wanakisiwa kuwa walihusika na kifo chake kilichotokea katika ajali mbaya ya barabarani. Ni lakabu inayohusishwa sana na vibaraka wanakodishwa na wanasiasa kuzua vurugu wakati wa mikutano ya wapizani wao au kuzuia vurugu wakati wanasiasa hawa wanapokuwa na

mikutano yao. Pia ni lakabu inayotumiwa sana na AbaGusii kuwarejelea vijana wanaopewa jukumu la kuchimba kaburi la mwenda zake na kuhakikisha kuwa amefukiwa vizuri kulingana na mila na desturi za AbaGagusii. Katika mchezo wa kandanda lakabu hii imeshuhudia badiliko la kisemantiki na sasa inamrejelea mchezaji mashuhuri ambaye hukodishwa na kulipwa ili kuchezea timu fulani. Wachezaji wengi wenye uzoefu na maarifa ya kucheza vizuri huwa wanajibandika au kubandikwa lakabu hii na mashabiki au wachezaji wenza.

41. *'Enkongo'* ni lakabu inayomaanisha mshindi (maana tambuzi). Enkongo katika jamii ya AbaGusii ni jina linalorejelea mshinda katika mchezo wa mieleka. Hivyo, maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji bigwa. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji shujaa ambaye alikuwa tegemeo la timu yake, kila alipoonekana uwajani ni kama tayari timu yake ilikuwa imejipatia ushindi.

42. *'Enchome'* ni lakabu inayomaanisha mtu mwerevu (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye akili. Hii ni lakabu ya majisifu. Mchezaji alijibandika ili kujigamba alivyo na akili nyingi au alivyo na busara kuwashinda wachezaji wengine.

43. *'Rikunyati'* ni mtu mjinga (maana tambuzi). Mashabiki kwa nia ya kuonyesha dharau au kutoridhika na mchezaji ambaye alikuwa haitekelezi kazi yake vyema, walimbatiza lakabu hii hasa pale ambapo alikuwa anaizuia timu yake kufunga mabao. Hivyo, maana ashirifu ni mchezaji asiyejua chochote (ashirifu).

44. *'Egiata'* ni mtu mwenye maumbile na akili iliyopambanuka (maana tambuzi). Ukamilifu wa mchezaji huyu kimaumble na kiakili ndivyo vigezo vinavyochangia kueleza maana ashirifu ya lakabu hii nayo ni mchezaji mkamilifu. Huyu ni mchezaji ambaye alikuwa na mwili mkubwa na maarifa ya kusakata kambumbu ilivyostahili.

4.2.3 Lakabu za wanyama wa mwituni, wanaofugwa na wa majini

Hizi ni lakabu zilizotokana na kufananisha wasifu wa mchezaji fulani pamoja na wasifu wa wanyama wa porini, wa kufugwa pale nyumbani na pia wale wanaoishi majini. Kwa mfano;

45. *'Enchogu'*. Ni mnyama mkubwa wa rangi ya kijivu mwenye mkonga, pembe mbili kubwa na masikio makubwa; ndovu (maana tambuzi) Maumbile ya mchezaji huyu ndiyo yaliyomfanya kubandikwa lakabu hii. Huyu ni mchezaji ambaye ni mrefu na mnene kama ndovu nambari tatu hadi nambari tano. Maumbile yake yalimpa uwezo na nguvu za kuzuia bao kufika kwenye lango lao. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye maumbile makubwa.

46. *'Agasusu'* ni mnyama mdogo mwenye miguu mifupi, masikio marefu ambayo husimama wima na mkia mfupi wenye manyoya mengi anayedaiwa kuwa mwerevu katika kuwakwepa maadui wake (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mjanja. Wasifu wa mnyama huyu katika hadithi za fasihi simulizi za Abagusii ndicho chimbuko cha lakabu hii. Kwa mujibu wa hadithi hizi licha ya maumbile aliyonayo mnyama huyu huwa anawashinda wanyama wengine kwa akili. Mashabiki walimbatiza lakabu hii mchezaji mwenye mwili mdogo lakini alikuwa na maarifa ya kucheza kandanda. Mchezaji huyu alikuwa hatari sana katika kuwachenga wachezaji wengine uwanjani.

47. *'Ebunda'*. Ni mnyama wa jamii ya farasi mwenye rangi ya kijivu lakini mdogo kuliko farasi na hutumiwa kuvuta mkokoteni au kubeba mizigo (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na wasifu wa mchezaji huyu kuwa mtundu na mkaidi. Ni mchezaji asiyependa kufuata maagizo na alipenda kufanya jinsi apendavyo uwajani. Hata hivyo aliposukumwa sana na wachezaji wengine au mashabiki aliweza kutoa kombora kali sana iliyotikisa wavu hivyo kuondolea timu yake mzigo wa aibu ya kushidwa na timu nyingine. Huyu ni mchezaji mkaidi (maana ashirifu).

48. '*Eng'iti*' ni mnyama wa msituni (tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji hatari sana. Maana hii inatokana na bidii ya mchezaji huyu wakati wa kucheza. Mchezaji huyu alifananishwa na mnyama mwitu kwa sababu yeye alikuwa hatulii hadi afunge bao. Mara nyingi alicheza nambari sita na alikuwa hachoki akiwa uwanjani.

49. '*Embeche*' ni mnyama mwitu wa jamii ya nguruwe mwenye meno mawili marefu yaliyochomoza nje ambaye hupenda kuishi mashimoni (maana tambuzi). Maumbile ya mchezaji huyu ndicho chanzo cha lakabu hii. Mchezaji huyu alifananishwa na ngiri kwa sababu meno yake ya mbele yalionekana kuchomoza sawa na yalivyo meno ya ngiri hivyo kuharibu wajihwa wa mchezaji huyu. Mchezaji huyu alikuwa na hasira sana. Kwa kurejelea sifa hizi zinazojitokeza maana ashirifu ya lakabu hii inajitokeza nayo ni mchezaji mwenye sura mbaya.

50. '*Enchoka*'. Maana tambuzi ya lakabu hii ni aina ya nyoka mwenye sumu kali ambaye hufurisha shingo wakati wa kutema mate yenye sumu kwa viumbe wengine; swila (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na mchezaji huyu kuwa tabia ya kuuficha mchezo wake na kuwashambulia wachezaji wengine bila wao kutarajia. Huyu ni mchezaji aliyekuwa na mbio sana hivyo haikuwa rahisi kumyanganya mpira uwanjani.

51. '*Esimba*'. Ni lakabu iliyotoholewa kutoka kwa jina la Kiwahili simba halafu likaambishwa kiambishi awali e-. Simba ni mnyama wa jamii ya paka, lakini mkubwa na mwenye rangi ya hudhurungi au majani makavu mwili mzima na alaye nyama (maana tambuzi). Jina asilia la EkeGusii ni *Endo*. Simba ni mnyama mkubwa na jasiri anayeaminika kuwa mfalme wa jangwani. Hivyo basi lakabu hii ilimrejelea mchezaji ambaye alikuwa shupavu na asiyemwogopa yeyote uwanjani. Ni mchezaji wa miraba minne aliyeogopwa sana uwanjani hasa aliposhika mpira kwani alikuwa na uwezo wa kuuchenga mpira na kuwapiku wachezaji wengine wote uwanjani. Katika fremu hii kuna ukubwa, ujasiri na ushujaa hivyo maana ashirifu ni mchezaji jasiri na shujaa.

52. '*Gechure*'. Ni mnyama mwitu anayefanana na mbuzi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye mbio na uwezo wa kuruka juu sana. Maana hii ilitoka na sifa ya mchezaji huyu ya kuweza kukimbia mbio sana uwanjani na pia uwezo wake wa kuruka na kutumia kichwa chake kuupiga mpira.

53. '*Enswa*' ni kiumbe wa majini aliye na mapezi na mkia ambavyo humwezesha kuogelea na mashavu yanayomwezesha kupumua akiwa majini; samaki (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na uwezo wa mchezaji huyu kufikiria kwa haraka na kutoa uamuzi kuhusu namna ya kuwapasha wenzake mpira uwanjani hasa alipokabwa na wachezaji pizani. Pia huyu ni mchezaji mwenye umaizi wa hali ya juu aliyefahamu kaida zote zinazohusiana na mchezo wa kambumbu. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye akili.

54. '*Enkonye*' samaki mrefu mwenye umbo la nyoka, huwa na rangi mbalimbali kama vile nyeusi, mabatobato ya chui, kijivu au kahawia; mkunga (maana tambuzi). Huyu ni mchezaji mjanja kama alivyo mkunga. Kila alipoushika mpira hakuna mchezaji mwingine aliyeweza kumpokonya. Pia haikuwa rahisi kumshika uwanjani, ni kama alikuwa akiteleza na kuponyoka mkononi kila wakati alipokabwa na wapinzani. Mchezaji huyu ni mstahimilivu na huwa hachoki wala kukata tamaa akiwa uwanjani hadi kipenga cha mwisho kilie.

55. '*Egesimba*' ni lakabu inayorejelea dhana tatu katika jamii ya AbaGusii kwanza, ni mnyama wa mwitu aliye mkubwa kama paka na anafanana na panya yeye hupenda kula kuku; ndezi. Pili hurejelea wavulana waliotahiri na mwisho inamaanisha kujificha. Asili ya lakabu hii ni tabia ya mchezaji huyu kuvizia na kuunyakua mpira bila wapizani kumuona kama afanyavyo ndezi anapotambua wanapolala kuku. Huyu ni mchezaji 'mwizi' (maana ashirifu).

56. '*Emamba*' ni mnyama kama kenge mkubwa mwenye magamba akaaye mtoni na ziwani; nywena (maana tambuzi). Huu ni utohozi jina halisi la EkeGusii ni *Enyangi* jina hili linatokana na ndoa baina ya

mwanamke mluo na mwanamme kutoka katika kijiji cha Bonchari kisha wakapata watoto. Mamba ni mnyama mkali na mwenye nguvu, kwa kawaida huwa hafanyi makosa hasa anapowinda windo. Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa mkali sana na mwenye nguvu na huwa makini sana hasa wakati wa kuchenga na kunyakua mpira. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mkali na mwenye nguvu.

57. '*Egesia*' ni mnyama wa porini anayefanana na mbuzi, mwebamba na mdogo, mwenye rangi ya kijivu na hudhurungi mgongoni, nyeupe tumboni, pembe ndefu kiasi na mkia wa kahawia na weupe nchani; paa (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa na mbio sana uwanjani licha ya kuwa na mwili mdogo. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye mbio sana.

58. '*Embori*' ni mnyama anayefanana na swala, anayefugwa kwa ajili ya kutoa nyama au maziwa (maana tambuzi). Huyu ni mchezaji anayependa kuvunja kanuni za mchezo wa kandanda, hata anapoonywa na kuelekezwa yeye huwa hatili maanani analoambiwa. Sifa ya mchezaji huyu kuwa mtundu na gaidi uwanjani ndicho kichocheo cha yeye kubatizwa lakabu hii na mashabiki. Hivyo, maana ashirifu ni mchezaji gaidi.

59. '*Echui*' ni mnyama wa msituni anayekula nyama ambaye anafanana na paka lakini mkubwa na mkali mwenye madoadoa ya njano na meusi (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa na ukali mwingi hasa wenye kudhalilisha. Huyu ni mchezaji mwenye mbio sana uwanjani. Pia yeye ni katili kiasi kwamba akikosa kuugoga mpira lazima atagoga mguu wa mchezaji mpizani, hivyo huogopwa sana uwanjani. Pia huitwa 'Engo' au 'Engonene'. Huyu ni mchezaji mkali na katili (maana ashirifu).

60. '*Egioto*' ni mnyama mdogo mwenye ngozi laini, asiye na mkia, ambaye anaruka sana, akaaye katika nchi kavu na katika maji (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa mfupi kwa kimo lakini mwenye uwezo wa kuruka sana kama afanyavyo chura. Mchezaji huyu alipopata mpira

haikuwa rahisi kupokonywa na wapizani. Maana ashirifu ni mchezaji mfupi na mwenye kuruka sana uwanjani.

61. '*Ribumburi*'. Ni mnyama wa porini anayefanana na ndezi ila ana mkia mrefu ulio na manyoa mengi. Yeye hula nyoka, Kuku na mayai (maana tambuzi). Katika jamii ya AbaGusii jina hili huhusishwa na kuiba pia hurejelea vijana wanaonyemelea wasichana. Lakabu hii ilibuniwa na mashabiki kumrejelea mchezaji mwenye mwili mkubwa ila ana tabia ya kufanya mambo kipumbavu. Maana ashirifu ni mchezaji mjinga.

62. '*Ekenyamato*' ni mnyama mdogo mwenye mbawa anayefanana na panya, hupenda kula matunda na wadudu na huruka usiku (maana tambuzi). Tabia ya mchezaji huyu ya kuzunguka uwanja mzima bila kuuguza mpira ndicho kichocheo cha yeye kubandikwa lakabu hii. Alipoingia uwanjani alikuwa kama kipofu hata alipobahatika kuuguza mpira aliupiga bila mwelekeo wowote. Sifa hii ya upovu ndiyo inayoelekeza maana ashirifu ya lakabu hii ambayo ni mchezaji kipofu.

63. '*Egechuchuti*' Maana tambuzi ya lakabu hii ni ana ya panya ambaye ni mdogo. Panya ni mnyama mdogo ila ni mharibifu sana hasa anapopata nafaka au nguo. Katika jamii ya AbaGusii jina hili hutumika kumrejelea mwanamke mwenye kelele na ugomvi kila wakati. Hivyo basi maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye kelele uwanjani iihali ni mharibifu na haisaidii timu yake kufunga mabao.

4.2.4 Lakabu za wadudu na ndege

Lakabu hizi zilitokana na kufananisha wasifu wa wachezaji na tabia mbalimbali zilizohusiswa na ndege au wadudu

4.2.4.1 WADUDU

64. '*Embogo*'. Maana tambuzi ya lakabu hii ni mdudu kama nzi mkubwa ambaye hufyonza damu ya mtu au mnyama na kumwambukiza maradhi ya malale au ugonjwa wa kusinzia. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mvivu na mtegemezi uwanjani. Chimbuko la lakabu hii ilikuwa ni tabia ya mchezaji huyu kuzembea uwanjani kiasi kwamba aliathiri utendakazi wa wachezaji wengine na kufanya juhudi zao za kufunga bao kuambulia patupu. Kutokana na uvivu wake alipoteza nafasi kadhaa za kufunga bao hivyo kuwafanya wachezaji wenzake kufa moyo na kukosa hamasa ya kucheza mpira kwa bidii.

65. '*Egesase*' Maana tambuzi ya lakabu hii ni mdudu wa jamii ya nzige mwenye mabawa na miguu minne, miwili ya mbele mifupi na miwili ya nyuma mirefu. Katika jamii ya AbaGusii wadudu hawa wakianza kuruka huashiria kuwa kuna siafu. Pia huashiria kuwa jua limekuwa kali. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye uwezo mkuu wa kuruka. Mashabiki wa mpira walimbandika mchezaji mwenye miguu mirefu lakabu hii. Kutokana na urefu wa miguu yake mchezaji huyu aliweza kuruka kwa ustadi uwanjani.

66. '*Enchoke*' ni mdudu atengenezaye asali, mwenye mabawa manne, huishi katika makundi na ana mwiba mdomoni autumiao kudungia maadui (maana tambuzi). Fremu zifuatazo zinajitokeza asali, ushirikiano katika makundi, bidii ya utendakazi. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwerevu na mwenye bidii. Usuli wa lakabu hii ni sifa ya mchezaji huyu kuwa na bidii uwanjani. Mashabiki walimbandika mchezaji huyu lakabu hii kutokana na werevu wake wakuwashirikisha wachezaji wenzake katika kutafuta mabao uwanjani. Ni mchezaji ambaye hutambua umuhimu wa umoja miongoni mwa wachezaji katika mchezo wa kandanda. AbaGusii wanaamini kuwa wadudu hawa wakiingia kwa nyumba utakuwa na mali.

67. '*Ensona*' ni mdudu mdogo mweusi anayeuma na anayeishi kwenye vumbi au manyoya ya wanyama wa nyumbani kama vile paka na mbwa (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni

mchezaji mwenye uwezo wa kujipenyeza kwenye upenyu mdogo na kunyakua mpira na kufunga bao. Chimbuko la lakabu hii ni maumbile ya mchezaji huyu alivyo mdogo lakini hatari sana kwa kujipenyeza kwenye ngome ya wapinzani na kuunyakua mpira hivyo kusababishia hasara.

68. '*Ensanako*' ni mdudu mwekundu wa jamii ya chungu lakini mdogo zaidi huishi na kutembea pamoja katika kundi na wenzake na huuma kwa uchungu sana (maana tambuzi). AbaGusii wanaamini kuwa msafara wa wadudu hawa ni ishara ya mvua kunyesha. Lakabu hii ilitokana na bidii ya mchezaji huyu ambaye aliunda kikoa na wachezaji wenzake na kuzuia mpira kufika kwenye lango lao. Hivyo basi maana ashirifu ya lakabu hii ni mlinda lango sugu.

69. '*Ribundu*' ni mdudu aina ya panzi ambaye huruka na hawezi kupaa (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mlegevu. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa goigoi uwanjani, huyu ni mchezaji asiyeweza kufanya uamuzi wa kipekee kuhusu kuokoa timu yake. Ni mchezaji mvivu ambaye kila mara lazima aelekezwe uwanjani.

70. '*Ekenyinyi*' ni mdudu wa majibaridi anayeng'ata na kujishikamanisha na mwili wa kiumbe kwa mfano mtu au mnyama na kufyonza damu (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji anayependa kuukwamilia mpira. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kugandia mpira anapoushika na inakua vigumu sana kwa wapinzani kumpokonya kwa sababu ya ujuzi wa hali ya juu alionao wa kuuchenga mpira.

71. '*Ritimbo*' ni mdudu ambaye hutoboa mbao (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mpumbavu. Mchezaji anayependa kuingilia mambo ya watu na kuyaharibu jinsi mdudu huyu anavyopenda kuingilia mbao na kuiharibu. Aghalabu, lakabu hii ilirejelea tabia ya mchezaji huyu kuharibu mpangilio wa mchezo na kuinyima timu yake nafasi ya kufunga bao.

72. '*Ekiarambe*' ni mdudu mkubwa mwenye mbawa na kiuno chembamba ambaye huuma kama nyuki; nyigu (maana tambuzi). Nyigu ni mdudu ambaye ana tabia ya kuuma kwa uchungu sana. Hivyo basi lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa na chuki kwa wachezaji wengine, ni mchezaji mwenye machungu mengi na aliweza hata kuwadhuru wachezaji wengine uwanjani. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mkorofi na mwenye chuki.

4.2.4.2 NDEGE

73. '*Engoncho*'. Maana tambuzi ni ndege mwenye rangi nyingi anayeweza kuiga maneno yanayosemwa na binadamu; Kasuku. Maana ashirifu ni mchezaji mpayupayu au mpayukaji. Mchezaji huyu hupenda kusema maneno yasiyokuwa na uzito au maana yoyote. Ni mchezaji mwenye kelele na kazi yake kuu uwanjani ni kuropoka maneno hivyo kuwafanya mashabiki kumbandika lakabu hii.

74. '*Egechibi*' ni aina ya ndege mdogo mwenye kelele nyingi; chiriku (maana tambuzi) Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kupenda kupiga kelele kila wakati hasa akiwa uwanjani hivyo mashabiki wakambandika lakabu hii. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii.

75. '*Egesami*' ni aina ya ndege mwenye mdomo mrefu na dhabiti uliopinda ambaye hula ndege wadogo na wadudu (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji jasiri katika kunyakua mpira Huyu ni mchezaji thabiti ambaye amebandikwa lakabu hii kutokana na tabia yake ya kuudhibiti mpira uwanjani.

4.2.5 Lakabu za mimea

Haya ni majina ya lakabu ambayo asili yake ni wasifu wa mchezaji unaonasibishwa na fremu mbalimbali zinazounda aina mbalimbali ya mimea inayopatikana katika sehemu za Gusii kwa mfano;

76. '*Ekenagwa*' ni aina ya mmea wenye miiba unaootesywa kwa lengo la kuwa ua ((maana tambuzi). Mmea huu uliletwa na wakoloni na ulianza kupandwa katika jamii ya AbaGusii mwaka

wa 1937. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mlinzi hodari. Hii inatokana na sifa za mmea huu ambao huwa na miiba na huota upesi na kuranda kote hivyo kuwa kizingiti kwa yeyote anayetaka kupenya kwenye ua.

77. '*Rikuneni*' ni matawi ya maharagwe yanayofanana na kunde na hutumika kama mboga (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mlinda lango bure kabisa. Maana hii ashirifu inatokana na sifa hasi za mmea huu. Mmea huu hutumika kama mboga wakati wa kiangazi. Hata hivyo huwa haupendwi na wanajamii kwa sababu inaaminika kuwa mama anayenyonyesha mtoto akila maziwa yatakauka pia husababisha maumivu ya tumbo na wakati mwingine humfanya mtu kushuta ovyo ovyo. Lakabu hii ilitumiwa na mashabiki kumrejelea mchezaji mlinda lango ambaye aliudhi sana kwa sababu alikuwa anafugwa mabao mengi kimaksudi. Mchezaji huyu alikuwa hana ladha tena uwanjani.

78. '*Emotii*' ni mti wenye pingili kama muwa lakini ulio na uwazi ndani na ambao matawi yake hutumika kama fito za kujeegea na pia kama mirija ya kuywea pombe ya kienyeji inayojulikana kama *Ebusaa* na shina lake hutumika kama bomba la kusafiria maji (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwembamba na mrefu ajabu. Hii ni kwa sababu Shina la mmea huu ni nyebamba, refu na thabiti. Lakabu hii ilitokana na maumbile ya mchezaji huyu ambaye ni mwembamba na mrefu ajabu. Kutokana na maumbile haya yake ni mchezaji ambaye ni thabiti na mwenye uwezo wa kudhibiti mpira uwanjani,

79. '*Egetugi*' ni sehemu ya mti kuanzia juu ya mzizi mpaka mwanzoni mwa matawi (tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mfupi na mnene. Lakabu hii ilitokana na maumbile na utendakazi wa mchezaji huyu ambaye hucheza nambari mbili au tano. Kazi yake kuu ni kuzuia wapinzani kufikisha mpira kwa mlinda lango. Huyu ni mchezaji matata ambaye mpira humpiti kabisa.

80. 'Masosa' ni matawi ya boga yanayotumiwa kama mboga (maana tambuzi). Mboga hizi hupendwa sana na abagusii. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji anayependwa sana. Mchezaji huyu huwa ni wa kutegemewa katika hali zote.

81. 'Rikongiro' ni magugu ya shambani yenye matawi makubwa yenye umbo la duara au duaradufu yanayoenea upesi na huliwa kama mboga hasa wakati wa kiangazi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwembamba na hafifu. Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuchoka haraka akiwa uwanjani. Huyu ni mchezaji mvivu sana na mtegemezi kama ulivyo mmea huu.

82. 'Enderema' ni aina ya mboga ya kijani kibichi inayoteleza na huwa na madini vitamin a,b,c (tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji legelege. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa mlegevu na mtegemezi. Kutokana na tabia yake ya kuchurupuka ni vigumu kutegemewa katika maamuzi ya kuokoa timu yake.

83. 'Egechachuti' ni majani au vijiti vilivyokauka vinavyotumika kuwashia moto (tambuzi). Tabia ya mchezaji huyu ya kuwatia ari ya kucheza wachezaji wengine ndicho kiini hasa cha lakabu hii. Huyu ni mchezaji ambaye ana uwezo wa kupanga mpira huku akiwashirikisha wenzake hadi ukatingiza wavu wa wapizani. Maana ashirifu ni mchezaji anayewamotisha wengine.

4.2.6 Lakabu zinazoonyesha matendo fulani

Hizi ni lakabu zinazoibuliwa na mashabiki wa mpira au mchezaji akajibandika mwenyewe kutokana na matendo fulani anayopenda kutenda. Kwa mfano;

84. 'Motarii' ni mtu anayetembea mahali pa kuvutia kwa ajili ya kuona mazingira na kujifurahisha (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji anayezururazurura uwanjani bila kuguza mpira. Hii ni sababu lakabu

hii huwa na asili yake katika tabia ya mchezaji huyu kukimbiakimbia uwanjani ovyo ovyo bila kuguza mpira ni kama anageuka na kuwa mtalii uwanjani badala ya kucheza mpira.

85. '*Ontimbu*' ni kuogelea majini (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji anayeshika mpira kwa mkono. Lakabu hii hutolewa na mashabiki kumrejelea mchezaji aliye na tabia ya kucheza mpira kwa kutumia mikono badala ya kutumia miguu hivyo kuifanya timu yake kuadhibiwa na kukosa nafasi ya kufunga bao.

86 '*Ribotabota*' ni tabia ya kufurafura uwanjani (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye tabia ya kununa uwanja. Mchezaji huyu alipenda kununa kila wakati hasa aliporekebiswa na wachezaji wenzake au kocha hivyo kuwafanya mashabiki kumbandika lakabu hii.

87. '*Kurura*' ni tabia ya kutumia nguvu ili kumfanya mtu au kitu kifuate kingine (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye ushawishi mkuu. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa na ushawishi mkuu kwa wachezaji wenzake. Ni mchezaji ambaye hubadilisha mkondo wa mpira kutokana na ujuzi wake wa kunyakua mpira kutoka kwa wachezaji pinzani na kuupiga kombora hadi kwenye lango la wapinzani.

88. '*Ekerambauti*' ni upepo wenye nguvu nyingi unaosababisha uharibifu wa kung'oa miti, mapaa na kutifua vumbi jingi; kimbuga (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji matata. Mchezaji huyu huwa na nguvu na pia huwa na ustadi wa hali ya juu wa kusakata kambumbu kiasi kwamba anapointia uwanjani ni kama kimbunga kwa sababu yeye husababisha uharibifu katika ngome ya wapinzani kwani kombora zake lazima zitikise wavu.

89. '*Egose*' ni hili ni tendo la kushtuka au kujivuta kidogo –mwili kwa sababu ya maumivu- kukwepa kando (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwoga (maana tambuzi). Lakabu hii inatokana na

tabia ya mchezaji huyu kujivuta uwanjani na kujiangushaangusha kila wakati uwanjani na kusababisha refa kusimamisha mpira.

90. '*Embeo egousa*' ni upeo unaovuma polepole bila athari yoyote (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mlegevu. Huyu ni mchezaji mlegevu kiasi kwamba kuwepo kwake uwanjani hakusababishi athari yoyote yaani mchezo haubadiliki kwa vyovyote vile. Mchezaji huyu ni mvivu na mlegevu ndio maana anafananiswa na upepo unaovuma polepole bila kuwa na athari yoyote.

91. '*Boyia*' ni tendo la kumvisha mtu nguo (maana tambuzi). Maana ashirifu yalakabu hii ni mchezaji mwenye kufunga mabao mengi. Lakabu hii inatokana na uwezo wa mchezaji huyu kufunga mabao mengi uwanjani. Huyu ni mchezaji ambaye amaaminiwa kuitolea timu yake aibu kwa kufunga mabao mengi.

92. '*Kururo*' ni kutumia nguvu kufanya mtu au kitu kifuate kingine. Kushawishi watu watende au wakubaliane na jambo fulani (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mlegevu. Lakabu hii inatokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa mlegevu na kujivuta sana akiwa uwanjani hivyo kuivuta timu yake nyuma.

93. '*Omosabi*' ni mwenye kupenda kuomba (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji asiyekuwa na doa kwa sababu lakabu hii inatokana na sifa ya mchezaji huyu kucheza kwa ustadi zaidi. Mara nyingi huwa ni mchezaji anayekopeswa au anayeombwa kutoka kwa timu nyingine mashuhuri na aliye na umahili wa kutosha wa kusakata kambumbu ili kusaidia timu iliyomuomba au kumkodisha kufaulu.

4.2.7 Lakabu zinazorejelea vitu mbalimbali

Hizi ni lakabu zinazobuniwa na mashabiki au wachezaji wa mpira kwa kufananisha tabia za mchezaji na vitu mbali vinayotumiwa kufanya kazi mbalimbali muhimu katika jamii. Kwa mfano;

94. '*Ebunia*' ni mfuko mpana na mrefu uliotengenezwa kwa nyuzi za kitani au katani kwa ajili ya kuwekea mazao au bidhaa kwa mfano maharage, mahindi, mchele na vitunguu (maana tambuzi). Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kucheza mpira kiholela holela. Mchezaji huyu alidhihirisha sifa ya gunia ambalo haliwezi kuaminika kufikisha mizigo salama kwa sababu ya tabia yake ya kuraruka ovyo ovyo na kuwaruhusu wadudu pamoja na panya kushambulia mzigo. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji asiyejua kucheza mpira.

95. '*Ensara*' ni kipande cha mti kilichotengenezwa vizuri na kuwekwa chuma chenye makali upande mmoja na unyoa wa kuku upande wa pili na kurushwa kwa upinde au kutiwa kwenye ziaka; mshale (maana tambuzi). Uwezo wa mchezaji huyu wa kukimbia kwa kasi akiwa uwanjani ndicho chanzo cha lakabu hii. Huyu ni mchezaji ambaye akipata mpira yeye huenda mbio sana na anapofika kwenye lango yeye hufunga bao kwa sababu kombora yake huwa inalenga ndipo. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwenye mbio sana.

96. '*Marionya*' ni nywele zinazoota kwenye mwili wa mnyama au ndege; manyoa (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mwepesi asiyekuwa na nguvu. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa mlegevu uwanjani kiasi kwamba anaweza kuyumbishwa kila mahali uwanjani na wachezaji wapinzani. Yeye ni kama unyoa unaoeperushwa na upepo kila mahali.

97. '*Ekegenga*' ni kipande cha mkaa au kuni ambacho kimeugua kiasi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji anayengaa sana uwanjani. Huyu ni mchezaji mwenye mbio sana na mwenye kutegemewa katika kusambaza mpira uwanjani. Pia ni mchezaji ambaye huwahamasa wengine kutia bidii uwanjani.

98. '*Oroteru*' ni kifaa kama sinia kilichotengenezwa kwa chane na hutumiwa kupepetea nafaka; uteo (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mnene. Lakabu hii ilitokana na wasifu wa mchezaji huyu kuwa na miguu ambayo ni kama imepanuka kiasi kwamba hawezi kuzuia mipira kupita.

99. '*Egesigisia*' ni kipande cha bomba au mti uliochomekwa ardhini ili kubeba uzito wa paa, dari ya nyumba au nyaya za umeme (maana tambuzi). Huyu ni mchezaji ambaye ndiye nguzo ya timu yake. Ni mchezaji tegemeo anayejua kanuni zote za kambumbu na mwenye ujuzi wa hali ya juu ya kusakata kambumbu. Hivyo maana ashirifu ni mchezaji mhimili.

100. '*Emesesi*'. Maana tambuzi ya lakabu hii ni dhana ya kitu kilichopondeka na kuwa ungaunga, vunjika na kuwa vipande vidogovidogo. Maana ashirifu ni mchezaji anayefanya kazi kwa bidii bila kupumzika. Lakabu hii iliashiria mchezaji huyu ana sifa ya kuwa mvumilivu hadi mwisho wa mchezo. Kule kuvumilia kupondwa hadi kuwa laini kabisa.

101. '*Rigombi*' ni utandu wa mafuta ulio juu ya maziwa ambao hutumika kutengeneza Siagi au samli; malai (maana tambuzi). Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji bora zaidi hii ni kwa sababu huyu mchezaji ambaye anategemewa sana na timu yake kwa sababu ya umahiri wake katika uchezaji wa mpira.

102. '*Richwati*' ni kitambaa kikubwa kilichozeeka na kurarukararuka (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mkogwe asiyeweza kucheza vizuri. Huyu ni mchezaji ambaye wakati fulani hasa alipokuwa kijana alikuwa na ujuzi mwingi wa kucheza mpira lakini sasa kwa sababu ya uzee yale makali yameisha hivyo anasalia kuwa kitambaa kikuukuu kinacholeta madhara ya kurarukararuka kinapotumiwa.

103. '*Rikorogoto*' ni kipande cha mti ambacho hufungiwa ng'ombe au farasi shingoni wakati wa kukokota gari au anapolima; nira (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mchezaji anayeaminika kuibeba timu yake. Lakabu hii ilitokana na bidii na kujitolea kwa mchezaji huyu wakati anapocheza. Huyu ni mchezaji aliyenasibishwa na timu, asipokuwepo au alipopata jeraha uwanjani basi matumaini ya timu hii kufaulu yalididimia.

104. '*Enkoba*' ni sauti kubwa inayoambatana na umeme inayosikika kutoka angani mvua inaponyesha; radi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye mbio ya ajabu. Lakabu hii ilitokana na uwezo wa

mchezaji huyu wa kukimbia kwa kasi ya ajabu na kuwapiku wachezaji wengine wote. Mchezaji huyu anapokuwa uwanjani, kasi yake inamfanya kutoonekana anapowapita wachezaji wengine. Sauti tu ndiyo husikika.

105. '*Ekebarabara*' ni pangaboi ndogo linalokuwa nyuma au mbele ya chombo cha majini ambalo likizunguka hukiwezesha chombo hicho kwenda; rafadha (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji anayewasukuma wengine mbele. Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu ya kuwasukuma wengine mbele. mchezaji huyu ni kama dira inayotoa mwelekeo wa mpira uwanjani.

106. '*Omosungose*' ni kamba inayotumika kuanikia nguo; mninginio (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji anayepitwa na mpira kwa urahisi. Mchezaji huyu ana sifa ya kutoweza kuuthibiti mpira. Kila mara anapopewa pasi yoyote huwa mpira unampita katikati ya mguu yake bila kuzuiliwa. Miguu yake imepanuliwa kama mninginio kiasi kwamba hawezi kuudhibiti mpira.

107. '*Egeuti*' ni kifuko kinachojazwa hewa na kupanuka ambacho watoto hupenda kuchezea na kutumiwa kama mapambo; baluni (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwepesi. Lakabu hii ilichochea na tabia ya mchezaji huyu kukosa udhabiti wakati wa kucheza mpira. Ni mchezaji ambaye anayumbayumba au kuyumbiswa na wachezaji wengine uwanjani.

108. '*Egosia*' ni mojawapo ya vazi linalovaliwa kichwani kwa nia ya kusetiri kichwa au kama pambo (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji maridadi. Huyu ni mchezaji anayependa kuvalia nadhifu akiwa uwanjani hata hivyo hana umahiri wa kusakata kabumbu. Yeye ni kama pambo uwanjani hivyo kuwafanya mashabiki kumbandika lakabu hii.

109. '*Ekeboye*' ni kifaa cha ujenzi kitumikacho kupigilia au kung'olea misumari; nyundo kubwa (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mfupi sana; mbilikimo. Kimo cha mchezaji huyu ndicho kichocheo

cha yeye kubandikwa lakabu hii. Huyu ni mchezaji ambaye ni mfupi na mnene ambaye husaidia sana hasa kuzuia mpira usiingie kwenye wavu.

110. '*Risasi*' ni kipande cha chuma au shaba chenye umbo la duara na ncha mbele na ambacho kina baruti ndani ambacho hulipuka na kufyatua ncha hiyo na kwenda kuiga kilicholegwa (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye kufyatuka mbio sana. Lakabu hii ilitokana na uwezo wa mchezaji huyu kuwa na kasi ajabu anapokuwa uwanjani.

112. '*Enguba*' ni kifaa bapa kilichotengeneza kwa ngozi, mti au kitu kingine cha madini chenye kishikio kati cha kujikinga na mishale au mikuki; ngao (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji stadi anayezuia mpira usifike kwenye lango. Mchezaji huyu ana uwezo wa kuzuia mipira kutingiza wavu au kumfikia mlinda lango. Sifa hii ndiyo kiini cha mashabiki kumbandika lakabu hii.

113. '*Rigena*' ni kipande kidogo kilicho meguka kutoka kwa mwamba au kitu chenye uzito maalum kilichotengenezwa kwa chuma kinachowekwa kwenye mizani kupimia uzito; jiwe (maana tambuzi). Huyu ni mchezaji mtundu asiyependa kufuata maagizo. Mchezaji huyu ni msumbufu asiyependa kuelekezwa. Yeye ni kama jiwe, haambiliki hasemezeki ndiposa mashabiki wakambatiza lakabu hii. Hivyo maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji mtundu.

114. '*Embombo*' ni kitu cha duara kinachotengenezwa kwa ngozi au vitu vingine ambacho hutumiwa katika michezo ya kandanda; mpira (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mnene na mfupi. Lakabu hii ilitokana na umbo la mchezaji huyu ambaye ni mnene na mfupi kiasi kwamba anaonekana kuwa na umbo la duara kama mpya.

115. '*Nyaanga*' ni mumiliki wa mavazi (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mpenda usafi. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kubadili mavazi yake kila mara.

116. ‘*Ekebondo*’ ni kibonyo kidogo hasa katika shavu au kidevu (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye kibonyo shavuni. Lakabu hii ilichochea na tabia ya mchezaji huyu kuwa na furaha na kutabasamu kila mara hasa akiwa uwanja.

117. ‘*Omochura*’ ni kulia kwa maneno yakukaripia ambayo ni makali (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye tabia ya kupiga kelele na kutoa maneno ya makali uwanjani. Huyu ni mchezaji mwenye hasira. Hasira humfanya kupiga kelele sana uwanjani hivyo kuchochea mashabiki kumpa lakabu hii.

118 ‘*Eubi*’ ni takataka, upuuzi au maandishi chapwa (maana tambuzi). Maana ashirifu mchezaji ovyo asiye na thamani. Lakabu hii ilitokana na mashabiki kukwazwa na namna mchezaji huyu anavyocheza mpira kipuzi na hivyo kumlinganisha na takataka inayohitajika kutupwa.

4.2.8 Lakabu za sehemu mbalimbali

Lakabu hizi zilibuniwa kutokana na kurejelea sehemu mbalimbali na manufaa yake kwa wanajamii. Kwa mfano:

119. ‘*Riiko*’ ni mahali pa kupikia (maana tambuzi). Katika jamii ya AbaGusii ‘*Riiko*’ ni sehemu muhimu sana. Mtoto mtundu na mtoro hukumbushwa kuwa ‘*Amaiga makorete*’ kumaanisha lazima njaa itamrejsha nyumbani. Mwanamke anaporuhusiwa kuwa na ‘*Riiko*’ huashiria kuwa amakubalika kama mke katika jamiii. Sehemu hii ikiharibiwa inamaanisha kuwa ndoa hiyo imevunjwa kabisa. Jikoni ni sehemu muhimu sana katika jamii yoyote ile. Lakabu hii ilitokana na umuhimu wa mchezaji huyu kwa timu yake. Huyu ni mchezaji ambaye ndiye kitovu cha ufanisi kwa timu yake, ndiye mchezaji anayepanga timu na kuelekeza pasi ambazo hutingisha wavu na kuzolea timu yake mabao mengi ya ushindi. Maana ashirifu ya la lakabu hii ni mchezaji shupavu.

120. *Ritundubari*’ ni sehemu inayotumika kupimia majani chai (maana tambuzi). Mchezaji huyu ni kama ‘*Etundubaru*’ yaani jumba kubwa lisilo na chochote kwa sababu linahitajika kuwa na hewa inayotosha ili kuzuia majani chai kuharibika. Mchezaji huyu hawezi kuzuia mipira kwa sababu mipira yote humpita kwa kweli hawezi kuisaidia timu yake kwa vyovyote vile. Maana ashirifu ya lakabu hii ni mchezaji asiyeweza kuzuia mpira.

121. ‘*Ekenya*’ ni ukingo wa barabara (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mlinda lango Huyu ni mlinda lango shupavu anayetegemewa na timu yake.

122. ‘*Ekeumbu*’ ni sehemu ya ardhi iliyo na rutuba ambamo uyoga na wadudu wanaoliwa hupatikana (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji nguzo ya timu yake. Huyu ni mchezaji tegemeo kwa timu yake. Yeye ndiye huwaongoza wengine wakati wa mazoezi na hata wakati wa mechi. Yeye ndiye hupanga mwelekeo wa mpira wakati wa mechi.

123. ‘*Etinga*’ ni sehemu ambamo mna mashine inayotumika kusagia unga (maana tambuzi). Maana ashirifu ni mchezaji mwenye nguvu. Lakabu hii ilitokana na maumbile ya mchezaji huyu ambaye ni mkubwa na mwenye nguvu. Mchezaji huyu alikuwa hachoki uwanjani hadi mechi ikamilike.

4.3 Mbinu zinazotumika kuunda lakabu

Sehemu hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kulingana na madhumuni mahususi ya pili ya utafiti huu nayo ni: kufafanua mbinu mbalimbali za lugha zinazotumika kubuni lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda. Ni muhimu kuelewa kuwa EkeGusii ni lugha mojawapo ya kibantu. Lugha za kibantu huwa ni lugha ambishi zinazotumia uambatishaji wa viambishi yaani viambishi awali, viambishi tamati pamoja na mashina au mizizi kuunda maneno.

4.3.1 Uundaji wa lakabu kutokana na nomino mbalimbali

Maumbo ya majina ya lakabu huathiriwa na mpangilio wa viambishi awali vya nomino mbalimbali katika lugha ya kibantu. Mapitio ya maandishi mengi kuhusu lugha za kibantu yanaonyesha kuwa nomino huainishwa katika seti zinazotambuliwa kama makundi ya nomino. Kuna makundi yasiyopungua ishirini na mbili yaliyotambuliwa (Welmer, 1973). Kila lugha ya kibantu huwa na seti nambari ishirini na mbili au idadi isiyopungua hii. Nomino huwa na misingi miwili: kiambishi awali na mzizi. Viambishi awali katika mengi ya makundi ya nomino huusisha irabu. Katamba (2003) anaeleza kuwa nomino huwekwa katika makundi mbalimbali kwa kutegemea vigezo vya kimsingi vya kisemantiki, kwa kutegemea kama inarejelea binadamu au viumbe wengine wenye uhai au kwa kutegemea wasifu wa kipekee wa nomino hizi kama vile ukubwa na umbo. EkeGusii kama lugha mojawapo ya kibantu ina makundi ishirini ya nomino (Cammenga, 2002) baadhi ya makundi haya ya nomino ni kama yafuatayo:

Kikundi	Mfano (umoja/wingi)	Fasiri ya Kiswahili
1. <i>Omo-</i>	<i>omo-nto</i>	‘mtu
3. <i>Omo-</i>	<i>omo-te</i>	‘mti’
4. <i>eme-</i>	<i>eme-te</i>	‘miti’
5. <i>eri-</i>	<i>eri-so</i>	‘jicho’
6. <i>ama-</i>	<i>ama-iso</i>	‘macho’
7. <i>eke</i>	<i>eke-moya</i>	‘mfuko’
9. <i>e-</i>	<i>e-kabira</i>	‘kabila’
9a. <i>e-n</i>	<i>e-nyigo</i>	‘figo’
10a. <i>ci-n</i>	<i>chi-nyigo</i>	‘figo’
11. <i>oro-</i>	<i>oro-ko</i>	‘kuni’

12. <i>aka-</i>	<i>aka-mura</i>	‘mvulana mdogo’
13. <i>oβo-</i>	<i>oβo-βa</i>	‘uyoga’
15. <i>oko-</i>	<i>oko-boko</i>	‘mkono’
16b. <i>a-</i>	<i>a-mate</i>	‘mate’

(Cammenga, 2002)

Katika lugha ya EkeGusii kiambishi awali cha nomino katika kikundi cha 1 na cha pili kinahusu nomino zinazorejelea binadamu katika umoja na wingi. Kikundi cha 9 na 10 kinahusu nomino zinazorejelea wanyama. Hata hivyo kuna nomino zinazohusu binadamu lakini zinapatikana nje ya kikundi cha 1 na cha 2. Kikundi cha 12 kinachohusiswa na viambishi *aka-* kinarejelea nomino katika hali ya udogo au hali ya kudunusha. Makundi haya ya nomino yanadhihirisha kuwa viambishi awali hubeba ujumbe kuhusu idadi na umbo la nomino, hata hivyo viambishi hivi awali sio muhimu sana katika kufanya maamuzi kuhusu makundi ya nomino ila kinachozingatiwa sana ni hulka ya nomino yaani iwapo inarejelea nomino zenye uhai au zile zisizo na uhai. Kwa upande mwingine watafiti wengi wa lugha za kibantu wanakubaliana kuwa, sifa muhimu zinazorejelewa wakati wa kuainisha nomino katika makundi ni: idadi, semantiki (iwapo ni binadamu, wanyama au vitu visivyo na uhai) na wakati mwingine kuweka kimakusudi bila kuzingatia sifa yoyote muhimu (Katamba, 2003).

Uhakiki wa data zilizokusanywa ulidhihirisha kuwa lakabu nyingi za wachezaji kandanda za lugha ya Ekegusii zimeundwa kutokana na nomino kwa kuzingatia mpangilio huu wa uainishaji wa nomino katika makundi kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

KIKUNDI	LAKABU YA EKEGUSII	FASILI YA KISWAHILI
<i>Omo-</i>	<i>Omong'ina</i>	Mama

	<i>omosongo</i> <i>mogiti</i> <i>omong'iti</i> <i>omochura</i> <i>omosabi</i>	mzungu fundi wa ua mchoyo mtu anayepiga unyenda mwombaji
1b. ∅		
<i>Aβa-</i>		
<i>Omo-</i>	<i>Omorambeka</i> <i>Omosungose</i>	Barabara mninginio
<i>Eme-</i>		
<i>Eri-</i>	<i>Ritimo</i> <i>risasi</i> <i>rikuneni</i> <i>rigena</i> <i>rigombi</i> <i>rikorogoto</i> <i>rigegu</i> <i>rigeto</i>	Mkuki risasi kunde jiwe malai nira jino kitu

	<i>rikongo</i>	ngombe mzee
	<i>richuma</i>	chuma
<i>Ama-</i>	<i>Amaiso</i>	Macho
	<i>Magoro</i>	Miguu
<i>Eke</i>	<i>Ekenagu</i>	Mwiba
	<i>ekenyamatu</i>	popo
	<i>egesase</i>	panzi
	<i>ekeboye</i>	nyundo
	<i>egeuti</i>	baluni
	<i>ekebarabara</i>	pangaboi
	<i>egesigisia</i>	ufito
	<i>ekegenga</i>	ukuni uliochomeka
	<i>egechibi</i>	chiriku
	<i>ekiarambe</i>	nyigu
<i>Eβi</i>		
<i>E</i>	<i>Embeche</i>	Ngiri
	<i>embombo</i>	mpira
	<i>emamba</i>	mamba

	<i>etinga</i>	tinga la kusaga unga
	<i>egosia</i>	kofia
	<i>emoti</i>	mwanzi
	<i>ebunia</i>	gunia
<i>a. e-n</i>	<i>Ensu</i>	Samaki
	<i>enchogu</i>	ndovu
	<i>enchoka</i>	nyoka
	<i>enchoke</i>	nyuki
	<i>ensona</i>	kiroboto
	<i>ensara</i>	mshale
	<i>engoncho</i>	kasuku
<i>Ci-</i>		
<i>a. ci-n</i>		
<i>Oro-</i>	<i>Oroteru</i>	Uteo
	<i>Ombogo</i>	mbung'o
<i>Aka.</i>	<i>Agasusu</i>	Sungura
<i>Obo</i>		
<i>Oko</i>		

b-a		
-----	--	--

Kwa kurejelea nomino katika kikundi cha kwanza (omo-) lakabu *Omong'ina* ilibuniwa kutoka kwa nomino ya Ekegusii *Mongina* inayomaanisha mama. Lakabu *Omosongo* ilitokana na nomino *Mosongo* inayorejelea mtu mweupe. Mfano mwingine ni lakabu *Mogiti* inayomaanisha mtu anayefanya kazi ya kujenga ua. Kutokana na maana hii, lakabu hii ilitumika kumrejelea mchezaji shupavu ambaye kazi yake ni kuzuia mpira isifike katika lango la timu yake. *Omong'iti* ni lakabu nyingine iliyoungwa kutokana na nomino ya Ekegusii *Mong'iti* iliyoamaanisha mchoyo. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kukataa kuwapa wachezaji wenzake nafasi ya kuucheza mpira kwa sababu alikuwa na tama ya kufunga bao ili apate sifa za kuitwa mchezaji bora.

Mfano mwingine ni lakabu *Omorambeka* inayomaanisha barabara. Lakabu hii ilitokana na urefu wa mchezaji huyu hivyo kumfananisha na barabara. *Ritimo* ni lakabu inayomaanisha mkuki, lakabu hii ilitokana na sifa za mchezaji huyu za kutoa kombora kali inayoogofya hata mlinda lango kiasi cha kuongopa kuzuia uwanjani hivyo kuchangia uundaji wa lakabu hii. Lakabu *Amaiso* iliudwa kutokana na nomino macho na ilimrejelea mchezaji ambaye macho yake ni makubwa kupita ya kawaida.

Mfano mwingine wa lakabu ya EkeGusii iliyoungwa kutokana na nomino ni lakabu *Ekenyamato*. Hii ni lakabu ambayo tafsiri yake ni popo. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kukimbia uwanjani bila kuuguzwa mpira, mchezaji huyu anafananishwa na popo kwa sababu yeye ni kama hauoni mpira. Hata hivyo, mengi ya majina haya ya lakabu yanachukua viambishi awali vinavyorejelea hali ya umoja kwa sababu lakabu hurejelea mchezaji mmoja ambaye anaweza kujibandika jina hilo au akabandikwa na mashabiki au wachezaji wenzake kama ilivyodhihirika katika jedwali.

Kama inavyodhihirika katika jedwali hili, katika kikundi cha kwanza kuna lakabu zinazotokana na nomino zinazohusu majina ya watu, Wanyama, ndege pamoja na wadudu wanaopatikana katika kikundi cha saba na tisa. Katika kikundi cha kumi na mbili kuna lakabu zinazotokana na nomino katika hali ya udogo hata hivyo lakabu nyingi zilizoundwa kutokana na nomino mbalimbali zilipatikana katika makundi mbalimbali ya uainishaji wa nomino bila kuzingatia sifa yoyote maalum, kilichozingatiwa ni viambishi awali vya majina haya ya nomino.

Mbinu nyingine iliyotumiwa kuunda lakabu ni mbinu ya kuunda lakabu kutoka kwa vitenzi kama ifuatavyo:

4.3.2 Uundaji wa lakabu kutoka kwa vitenzi

Lakabu za wachezaji kandanda zinaweza kuundwa kutoka kwa vitenzi mbalimbali kwa mfano; *Motari* mtalii ni lakabu inayotokana na mzizi wa kitenzi '*tara*' inayomaanisha kutembea na kiambishi nafsi '*mo-*'

Lakabu hii inamrejelea mchezaji aliye na tabia ya kukimbia ovyoovyo uwanjani bila kuguza mpira kama afanyavyo mtalii anapozuru sehemu Fulani. *Ribotabota* ni lakabu inayomaanisha mwenye kununa. Lakabu hii ilitokana na kitenzi '*-bota*' inayomaanisha kuvimba pamoja na kiambishi ch ngeli '*ri-*'. *Kururo* vuta ni lakabu inayoundwa kutokana na kitenzi '*kurura*' inayomaanisha kuvuta. *Ogose* ni lakabu inayomaanisha mwoga. Ni lakabu inayoundwa kutokana na kitenzi '*gosa*' inayomaanisha kushtua pamoja na kiambishi cha nafsi. *Omosabi* mwombaji ni lakabu inayoundwa kutokana na kitenzi '*saba*' omba.

Enterere ni lakabu inayomaanisha telezi. Lakabu hii iliundwa kutokana na kitenzi *terera* teleza. *Okemanyi* mjuaji ni lakabu inayoundwa kutokana na kitenzi '*manya*' jua. *Otwoma* mgongaji ni lakabu inayoundwa kutokana na kitenzi '*twoma*' gonga pamoja na kiambishi cha nafsi *o-*. Kutokana na utafiti huu wa sasa ilidhihirika kuwa lakabu hizi zilizotokana na vitenzi huundwa kwa kuambisha kiambishi awali cha nafsi pamoja na mzizi wa kitenzi hivyo kuibua lakabu hizi.

4.3.3 Muundo wa sentensi

Sentensi ni utungo ulio na kiima pamoja na kiarifa. Utafiti huu uligundua kwamba baadhi ya lakabu zilizoainishwa zina muundo wa sentensi. Hizi ni lakabu ambazo kimaumbile zilionekana kama kishazi au sentensi kwa sababu zilikuwa na kiima na kiarifa. Kwa mfano: *Embeo egousia* ni lakabu iliyoungwa kwa kiima 'Embeo' iliyomaanisha upepo na kiarifa 'egousia' iliyomaanisha upepo unaovuma. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji ambaye hakuwa na nguvu ya kukimbia uwanjani yeye ni kama upepo unaovuma na badala ya kuisaidia timu yake yeye hupoteza muda uwanjani.

4.3.4 Lakabu zinazoudwa kutokana na mbinu ya ukopaji

Kukopa ni tendo la kuchukua istilahi ya lugha fulani na kisha kuitumia kama istilahi katika lugha nyingine (Kiango, 2002). Kukopa ni mojawapo ya mbinu ya kiisimu ambayo hutumiwa na lugha zote ulimwenguni kuunda istilahi na maneno mapya ili kukidhi mawasiliano katika miktadha anuwai. Baadhi ya lakabu katika utafiti huu zimeibuka kutokana na mbinu hii ya ukopaji. Mathalani: Lakabu *Ebunia* imeundwa kutokana na neno la lugha ya Kiswahili -gunia-. Mbinu ya ukopaji iliyotumika ni utohozi ambapo maneno kutoka lugha chanzi hukopwa na hatimaye hufanyiwa marekebisho kwa kufuata kaida au sheria za kifonolojia za lugha pokezi kabla ya kutumiwa. Hivyo basi, neno la Kiswahili gunia 'limeGusiilishwa' na kuwa egunia. Neno linalokopwa hutamkwa na kuandikwa kwa utaratibu wa lugha pokezi.

Lakabu *Echabu* imeundwa kutokana na mbinu hii ya ukopaji. Hii ni lakabu inayotokana na neno la Kiswahili uchafu inayorejelea mchezaji ambaye hana faida yoyote uwanjani. Lakabu *Ebunda* ilibuniwa kutoka kwa neno la Kiswahili punda, lakabu hii inarejelea mchezaji mtundu ambaye hapendi kufuata maagizo anayopewa uwanjani. Lakabu *Richuma* inatokana na neno la Kiswahili chuma ambalo hubandikwa mchezaji ambaye ndiye tegemeo la timu. Mara nyingi huwa ni mchezaji wa kulipwa aliye na tajriba ya hali ya juu katika mchezo wa kandanda. Lakabu *Ochusi* ilibuniwa kutoka kwa neno la Kiswahili

ujuzi lakabu hii ni ya mchezaji ambaye aliaminika kuwa na ujuzi wa hali ya juu katika mchezo wa kandanda. Lakabu *suru* ilitokana na neno la Kiswahili haidhuru ambalo lilipokopwa matamshi yake yalibadilika kutokana na athari ya matamshi ya maneno katika lugha ya Ekegusii. Mbinu nyingine inayotumiwa katika uundaji wa lakabu za Ekegusii ni mbinu ya ufupishaji.

4.3.5 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya ufupishaji

Ufupishaji ni mbinu ambayo hutokana na kitenzi ‘fupisha’ chenye maana ya kufanya kitu kiwe kifupi au kupunguza urefu wa kitu. Kuna mbinu mbalimbali ambazo zinatumika katika ufupishaji ili kuunda maneno mengine mapya. Kwa mfano: Lakabu *Mura* iliundwa kupitia matumizi ya mbinu ya ufupisho mkato kutoka kwa neno *Omomura* lenye maana ya mvulana barobaro. Katika mbinu hii ya ufupisho mkato baadhi ya vipashio au silabi hudondoshwa kabisa na kuacha sehemu tu ya neno asilia. Mfano mwingine wa lakabu iliyoungwa kwa kutumia mbinu ya ufupishaji ni Lakabu *suru* ambayo ilitokana na kutohoa neno la Kiswahili ‘haidhuru’ kisha kwa kutumia mbinu ya ufupisho mkato neno hili likafupiswa hadi ‘*suru*’.

4.3.6 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya uradidi

Uradidi ni utaratibu unaotumika katika kuunda maneno ambayo sehemu ya neno lote hurudiwa ili kuunda neno jipya au msisitizo fulani (Matinde, 2012). Kwa mfano: Lakabu ‘*Ribotabota*’ imeundwa kutokana na kurudia kitenzi ‘*bota*’ inayomaanisha kuvimba au kufura. Neno hili linasisitizwa kwa kurudia ‘*botabota*’ hivyo kupata maana iliyotarajiwa ya kuonyesha mazoea ya kufura, kuvimba au kununa kila wakati. Lakabu nyingine iliyoungwa kwa kutumia mbinu hii ya uradidi ni lakabu *Ritukutuku*, lakabu hii inatokana na uradidi kamili wa sauti ‘*tuku*’ ili kuonyesha mlio unaotolewa na injini inapowashwa. Uradidi huu unasaidia kuunda taswira hivyo kuelewa maana ya lakabu hii.

4.3.7 Uundaji wa lakabu kutokana na mbinu ya uambatanishaji

Uambatanishaji ni mbinu ambayo huhusisha kuunganishwa kwa maneno mawili kuunda neno moja jipya ambalo maana yake huwa tofauti na maneno ambayo yametumika kuunda neno hilo. Kwa mfano; ‘*Enda*’ (tumbo) + ‘*Emwamu*’ (nyeusi) inaunda neno jipya ‘*Endamwamu*’ (tumbojeusi) inayomaanisha mtu mwenye wivu uliokithiri mipaka. Maana hii mpya ni tofauti sana na maana ya maneno yaliyotumika kuunda neno hili. Kutokanana mbinu hii ya kuambatisha nomino ‘*Enda*’ na kivumishi ‘*Emwamu*’ lakabu ‘nyandamwamu’ huudwa.

4.3.8 Uundaji wa lakabu kwa kutumia mbinu ya uhamishaji

Matinde (2012) anaeleza kuwa uhamishaji (pia upanuzi wa maana) ni mbinu ambayo maana ya neno hupanuliwa na kurejelea dhana tofauti. Hata hivyo, upanuzi huu huzingatia fahiwati zilizomo katika neno la kwanza na kujaribu kuzioanisha na maana, umbo, tabia na uamilifu wa neno la pili. Lakabu nyingi zilizotumika katika utafiti huu zilibuniwa kwa kutumia mbinu hii ya uhamishaji kwa mfano: lakabu *Omorambeka* ni neno la lugha ya Ekegusii linalorejelea barabara iliyonyooka. Kama lakabu maana hii ya barabara imehamiswa ili kurejelea mchezaji mrefu sana. *Nyataya* ni neno linalomaanisha taa. Kama lakabu maana imehamiswa na kurejelea macho kuashiria kuwa huyu mchezaji ana macho ya ajabu yasiyo ya kawaida. Pia hutumika kumaanisha kuwa mchezaji huyu ndiye mwanga wa timu yake yaani ni yeye ambaye ni tegemeo au uti wa mgongo wa timu yake.

Embombo ni neno linalorejelea mpira. Kama lakabu maana imehamiswa na kurejelea mchezaji mfupi na mnene ambaye anaonekana kufanana na umbo la mpira. *Embiro* ni neno linalomaanisha masizi, kutokana na rangi nyeusi ya masizi maana iliamishwa ili kurejelea lakabu iliyomaanisha mtu mweusi. *Omosongo* ni neno linalomaanisha mzungu. Kama lakabu maana hii imehamiswa na kurejelea mchezaji mweupe pepepe kutokana na sifa ya rangi ya mzungu. *Ebunda* ni neno linalomaanisha mnyama anayeitwa punda. Huyu ni

mnyama mkaidi sana, hivyo basi kama lakabu maana huamishwa ili kumrejelea mchezaji mtundu na mkaidi asiyependa kufuata maagizo uwanjani.

Rikuneni ni neno linalomaanisha matawi ya maharage yanayofanana na kunde na hutumika kama mboga. Mboga hizi huwa hazipendwi sana kwa sababu mara nyigi humfanya mtu kuumwa na tumbo hivyo kumzuia kufanya kazi zake za siku kama kawaida. Kama lakabu maana huamishwa na kumrejelea mlinda lango asiyeweza kudhibiti kazi yake na kufungwa mabao mengi sana uwanjani. Lakabu nyingine iliyoundwa kutumia mbinu ya uhamishaji ni lakabu *Ritundubari* ambayo inamaanisha sehemu inayotumiwa kwa shughuli za kupimia majani chai. Kwa kawaida huwa ni sehemu iliyowazi ili kuruhusu hewa nyingi kwa sababu joto jingi huharibu majani chai. Kama lakabu maana imehamishwa kwa kuzingatia sifa hii ya uwazi ili kumrejelea mchezaji asiyeweza kuzuia mpira kumpita. Mipira humpita jinsi hewa hupita ndani ya '*Tundubari*' bila kuzuiliwa.

4.4 Matumizi ya lakabu katika mchakato wa kucheza kandanda

Sehemu hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kulingana na madhumuni mahususuya tatu ya utafiti ambayo ni; kupambanua matumizi ya lakabu za EkeGusii katika mchakato wa kucheza kandanda. Uchanganuzi wa maana ya lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda unadhihirisha kuwa kitamaduni na kijamii maana ya lakabu ni muhimu. Maana hii huathiri namna mchezaji atakavyocheza mpira uwanjani kwa sababu lakabu hudhihirisha iwapo mtumizi wa lakabu anakubaliana au anaudhika na wasifu wa anayemlakabu pia huwasaidia wachezaji kandanda kujithathimini ili kuelewa msimamo wa mashabiki kuhusu mchezo wao ndiposa waweze kujibidiisha zaidi.

Lakabu hutumika katika mawasiliano baina ya wanajamii hivyo ni kiungo muhimu sana katika kufafanua urasmi au ukaribu wa mahusiano baina ya wanajamii. Hivyo ni njia mojawapo ya wazi ya kufafanua mahusiano yaliyopo baina ya wachezaji mpira na mashabiki wao.

Lakabu hutumika kumdunisha na kumdhalilisha mchezaji na hivyo kuathiri kwa njia hasi namna anavyocheza mpira uwanjani. Kwa mfano mchezaji anayebandikwa na mashabiki mahasidi lakabu ‘*Agasusu*’ inamaanisha kuwa mashabiki wanamuona kama kijisugura hivyo kumaanisha kuwa ana ujanja lakini ujanja wake ni mdogo na hawezi kuisaidia timu yake. Matumizi ya kiwakilishi awali /aka-/ cha uainishaji nomino katika kundi la 12 kunakusudiwa kumdhalilisha aliyebandikwa lakabu au kumfanya kuonekana asiyekuwa na thamani.

Lakabu nyingine za EkeGusii zinazodhalilisha na kumvunja moyo mchezaji ni kama lababu ‘*Eubi*’ inayomaanisha takataka. Kwa kweli inaudhi sana mchezaji anapocheza uwanjani halafu anagundua kuwa ni yeye anayelitwa takataka. Lakabu hii hubuniwa na mashabiki hasa wanaoashabikia timu anayocheza mchezaji huyu na huonyesha wamekwawa na uchezaji wa kipuuzi wa mchezaji huyu na hivyo kumuona kama takataka inayostahili kutupwa yaani anastahili kutolewa uwanjani na mchezaji mwingine kuchukua nafasi hiyo yake. Mchezaji huyu hana budi ila kutia bidii ili kubadili anavyocheza mpira ili awe kubadili msimamo wa mashabiki kumuhusu.

Lakabu hutumika kumsifu mchezaji na hivyo kumpa hamasa ya kutia bidii uwanjani. Kwa mfano matumizi ya lakabu ‘*Enchogu*’ inayomfananisha mchezaji na ndovu huonyesha kuwa mashabiki wanapendezwa na maumbile ya mchezaji huyu ambaye kutokana na mwili wake mkubwa na nguvu nyingi alizonazo hucheza nambari tatu, nne au tano na kazi yake kuu ni kuchunga mpira usikaribie wavu. Mfano mwingine ni lakabu ‘*Egioto*’ lakabu hii inamaanisha chura na hutumiwa na mashabiki kumsifia mchezaji ambaye ni mfupi kwa kimo lakini anajibidiisha na kunoa uwezo wake wakuruka na kuudhibiti mpira hivyo kuisaidia timu yake. Mchezaji anaposikia akiitwa lakabu za aina hizi yeye hujibidiisha ili kuwafurahisha mashabiki. Lakabu hizi pia huwa ni za majingambo na mchezaji mwenyewe anaweza kujibatiza na akafurahia matumizi yake hata nje ya mktadha wa mchezo wa kandanda.

Matumizi mengine ya lakabu ni kuchochea ushirikiano baina ya wachezaji wanapokuwa uwanjani. Kwa mfano lakabu *'Enchoke'* ni lakabu inayomaanisha nyuki. Kwa kurejelea mhimili wa nadharia ya semantiki ya fremu, katika fremu ya mdudu nyuki kuna sifa kama vile bidii, ushirikiano, kujitolea mhangana kwa niaba ya wengine na utenda kazi. Hivyo basi hii ni lakabu inayotokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa na bidii uwanjani. Mashabiki walimbandika mchezaji huyu lakabu hii kutokana na werevu wake wa kuwashirikisha wachezaji wenzake katika kutafuta mabao uwanjani. Ni mchezaji ambaye anatambua umuhimu wa umoja miongoni mwa wachezaji katika mchezo wa kandanda. Lakabu nyingine inayoonyesha ushirikiano ni *'Ekegenga'* ambayo ni kipande cha mkaa au kuni ambacho kimeungua kiasi. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji mwenye mbio sana na mwenye kutegemewa katika kuwasambazia wachezaji wengine mpira uwanjani na hivyo kuchangia kufunga bao.

Aghalabu lakabu hutumika kukejeli na kukashifu uvivu wa baadhi ya wachezaji uwanjani. Kwa mfano lakabu *'Ritukutuku'* ni lakabu inayorejelea mchezaji ambaye hakimbii uwanjani hasa mashabiki wanapomtarajia akimbilie mpira ndipo apeane pasi kwa haraka au anapohitajika kukimbia ili kuokoa mpira usigoge wavu. Lakabu hii imebuniwa kutokana na tanakali ya sauti inayoiga sauti inayotolewa na injini inapowaswa. Hivyo, kasi ya mchezaji huyu inafananishwa na sauti hiyo mbovu ya kukereketa sikio na pia muda mrefu unaotumika kutoa sauti ya *'tukutuku'* inayotolewa na injini hii. *'Kururo'* ni lakabu iliyotokana na tabia ya mchezaji huyu kuwa mlegevu na kujivuta sana akiwa uwanjani na hivyo kuivuta timu yake nyuma.

Lakabu *'Embeo egousa'* ni lakabu inayomaanisha upepo unaovuma polepole bila madhara yoyote. Lakabu hii hutumiwa na mashabiki kumkashifu mchezaji huyu mlegevu anayecheza kivivu kiasi kwamba kuweko kwake uwanjani hakusababishi athari yoyote yaani mchezo haubadiliki kwa vyovyote vile. Lakabu *'Ombogo'* inamrejelea mchezaji mvivu na mtegemezi uwanjani. Lakabu hii inatokana na tabia ya mchezaji

huyu kuzembea kiasi kwamba anaathiri utendakazi wa wachezaji wengine na kuzima zuhudi zao za kufunga bao.

Fauka ya hayo, lakabu nyingine inayohusu uvivu ni lakabu '*Rikuneni*' hii ni lakabu inayorejelea matawi ya maharagwe yanayofanana na kunde na hutumika kama mboga hata hivyo mboga hizi huwa hazina ladha nzuri na wakati mwingine husababisha matatizo ya kuumwa na tumbo. Ni lakabu inayotumiwa na mashabiki mahasidi kumkejeli mlinda lango mvivu ambaye anafugwa mabao kiholela kuashiria kuwa hana thamani yoyote kwa timu yake. Matumizi ya lakabu hizi za kukejeli na kukashifu huwaathiri sana wachezaji hawa wanaobandikwa lakabu hizi hasi kiasi kwamba wengine wao (wakati mwingine) huwa na hasira na kuzua vurugu uwanjani hivyo kuharibu mechi au kufanya timu zao kupigwa faini. Wakati mwingine wachezaji hawa wanapogundua kuwa lakabu hizi zinawarejelea huwa kama kichocheo cha kuwafanya kutia bidii uwanjani ili kuokoa hadhi zao kama wachezaji wa kandanda.

Lakabu hutumika kujasirisha na kuwatia shime wachezaji wanaotia bidii uwanjani kwa mfano lakabu '*Esimba*' ni lakabu ya mchezaji jasiri na shujaa. Lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa shupavu na asiyemwogopa yeyote uwanjani. Lakabu hii humfanya mchezaji huyu kujihisi yeye ndiye mfalme pale uwanjani hivyo kujibidiisha ili aendeleo kusifiwa na mashabiki. Lakabu '*Emamba*' ni lakabu nyingine ya kujasirisha. Lakabu hii huwa ni ya majingambo na ilitokana na sifa ya mnyama mamba ambaye huwa hafanyi kosa anapowinda windo. Hivyo basi mchezaji anaposikia mashabiki wakimsifia kwa kumwita lakabu hii yeye hujizatiti ilikuhakikisha hapotezi nafasi ya kufunga bao. Mfano mwingine ni lakabu '*Egesami*' hii ni lakabu inayomaanisha aina ya ndege mwenye mdomo dhabiti uliopinda. Lakabu hii ilimrejelea mchezaji jasiri na thabiti mwenye uwezo wa kuudhibiti mpira uwanjani kama afanyavyo ndege huyu anapopata windo.

Kwa kuongezea, lakabu hutumika kuonya hasa wachezaji wasiofuata maagizo. Kwa mfano lakabu '*Embori*' ni lakabu inayomaanisha mbuzi. Lakabu hii huchochewa na sifa ya mchezaji huyu kuwa mtundu

na gaidi. Huyu ni mchezaji anayependa kuvunja kanuni zote za mchezo wa kandanda na hata anapoonywa yeye huwa hatilii maanani na mwishowe huadhibiwa na kuigharimu timu yake. Mfano mwingine ni lakabu *'Ebunda'* lakabu hii inatokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa mkaidi kama punda, ni mchezaji asiyependa kufuata maagizo. Wakati mwingine inabidi wachezaji wenzake wamzomee hivyo kusababisha ugomvi uwanjani. Ukaidi wa wachezaji hawa huathiri sana utendakazi wao kiasi kwamba wanaweza kuathiri kwa njia hasi matokeo ya timu kwa ujumla.

Lakabu hutumika kuonyesha maumbile ya kipekee yasiyo ya kawaida ya baadhi ya wachezaji kandanda kwa mfano lakabu *'Matacho'* ni lakabu inayoonyesha kuwa mchezaji ana miguu mikubwa isiyo ya kawaida. Ukubwa wa miguu ya mchezaji huyu humsaidia kudhibiti mpira na hivyo kuwababaisha wachezaji wengine uwanjani. Mfano mwingine ni lakabu *'Gekuba'* lakabu hii ilimrejelea mchezaji ambaye alikuwa na kifua kikubwa sana ambacho yeye alikitumia kwa ufasaha katika kupiga mpira. Lakabu nyingine ni *'Matogoro'* ni lakabu inayoashiria mchezaji ana macho makubwa yasiyokuwa ya kawaida. Mchezaji huyu alikuwa na tabia ya kukondoa macho na kuwashtua wachezaji wengine. Mfano mwingine ni lakabu *'Nyamioro'* lakabu hii ilitokana na sifa ya mchezaji huyu kuwa na mwili mdogo lakini pua kubwa lisilokuwa la kawaida hivyo kumtambulisha hata akiwa mbali. Mfano mwingine ni lakabu *'Nyamotwe'* lakabu hii ilitokana na mchezaji huyu kuwa na kichwa kikubwa ajabu. Mchezaji huyu hutumia kichwa hiki chake kupigia mpira. Lakabu hizi zinazoshabikia upekee wa maumbile ya wachezaji hawa huwapa ari ya kuendelea kujikaza wanapokuwa uwanjani hivyo kuisaidia timu yao kushinda.

Lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda hutumika kuonyesha msimamo wa Abagusii kuhusu masuala fulani katika jamii kwa mfano lakabu *'Omongina'* ni lakabu inayotumika kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Lakabu hii ilitokana na tabia ya mchezaji huyu kuzembea uwanjani. Uzembe huu humfanya mchezaji huyu kukejeliwa na mashabiki kwa kuitwa mama mkogwe. Mama ambaye amefikisha kikomo cha hedhi hivyo hatarajiwi tena kuzaa. Huyu mchezaji ni mzembe na hana makali tena ya kuisadia timu

yake. Lakabu hii hubuniwa na mashabiki hasidi kwa nia ya kumdhalilisha mchezaji huyu. Pia humfanya mchezaji huyu kupandwa na mori na kukosa umakini uwanjani.

Riiko ni mahali pa kupikia. Katika jamii ya AbaGusii ‘*Riiko*’ ni sehemu muhimu sana. Mtoto mtundu na mtoro hukumbushwa kuwa ‘*Amaiga nakorete*’ kumaanisha lazima njaa itamrejeshwa nyumbani. Mwanamke anaporuhusiwa kuwa na ‘*Riiko*’ huashiria kuwa amekubalika kama mke katika jamii hii. Sehemu hii ikiharibiwa inamaanisha kuwa ndoa hiyo imevunjwa kabisa. Jikoni ni sehemu muhimu sana katika jamii yoyote ile. Lakabu hii ilitokana na umuhimu wa mchezaji huyu kwa timu yake. Huyu ni mchezaji ambaye ndiye kitovu cha ufanisi kwa timu yake, ndiye mchezaji anayepanga timu na kuelekeza pasi ambazo hutingisha wavu na kuzolea timu yake mabao mengi ya ushindi. Maana ashirifu ya la lakabu hii ni mchezaji shupavu.

Lakabu nyingi zilizotumika zinaonyesha kuwa Abagusii ni wakulima na wafugaji. Chakula wanachokipenda ni ugali kwa sababu wanamshabikia mchezaji mwenye nguvu na kumbandika lakabu ya sehemu ya kusiagia unga (*Etinga*) na mboga mbalimbali kwa mfano *Enderema*, *Masosa*, *Rikuneni* na mengineo. Pia ni watu watarabu wasiopenda uchafu ndiposa wanamlakabu mchezaji anayecheza vibaya ‘*Eubi*’ –takataka na hivyo wanashabikia usafi kwa kumsifia mchezaji anayeonekana kuwa maridadi na kumbandika lakabu ‘*Nyaanga*’ na kusisitiza umuhimu wa kutia bidii.

Lakabu nyingi zilizotumika katika mchakato wa mchezo wa kandanda ni muhimu sana kwa sababu zinaonyesha matukio muhimu katika historia ya AbaGusii. Kwa mfano lakabu kama vile ‘*Matacho*’ maana yake kulingana na maarifa yaliyomo kwenye akili ya AbaGusii inarejelea miguu mikubwa kama ya ndovu. Dhana hii ilitokana na misafara ya ndovu ya mwaka wa elfu moja mia tisa hamsini na nane walioingia Gusii sehemu ya Gesabakwa kutoka mbuga ya wanyama ya Maasai Mara kuelekea mji wa Tanzania ‘*Ekenagwa*’ ni lakabu inayomaanisha aina ya mmea wenye miiba unaooteshwa kwa lengo la kuwa ua.

Mmea huu uliletwa na wakoloni na ulianza kupandwa katika jamii ya AbaGusii mwaka wa elfu moja mia tisa thelathini na saba.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ya tano na ya mwisho inatoa muhtasari wa hoja zote muhimu zilizojadiliwa katika matokeo ya utafiti na kutoa mapendekezo kuhusu sehemu zinazostahili kufanyiwa uchunguzi na utafiti zaidi baadaye.

5.2 Hitimisho

Kidokezo cha lakabu katika jamii ya AbaGusii huwasilisha maana hasi au chanya. Katika utafiti huu imebainika kuwa Lakabu huwa na maana mbalimbali. Semantiki ya lakabu hizi, ikijumuishwa na hali ya kitamaduni na kijamii ni chimbuko la lakabu za EkeGusii. Hivyo basi matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha wazi kuwa majina ya lakabu ya wachezaji kandanda ya EkeGusii kama yalivyo majina mengine ya kiafrika yana thamani ya kisemantiki: maana tambuzi na maana ashirifu.

Maana hii tambuzi na maana ashirifu huibuliwa kwa kuchunguza asili ya lakabu hizi sawa na alivyofanya Olenyo (2011) katika utafiti wake aliokuwa akichunguza semantiki ya majina ya Walogoli wanaoishi nchini Kenya. Ithibati zaidi ilijitokeza katika utafiti wa Swian (1957) aliyeshikilia msimamo kuwa tabia na hulka mbalimbali zinazohusishwa na jina na fasili yake iliyo akilini ndiyo hufanya jina hilo kuwa na maana. Upungufu wake ulikuwa kutotaja fasili hizi: maana tambuzi na maana ashirifu. Kwa kuzingatia marejeleo na fasili iliyo akilini mwa mtu, lakabu za EkeGusii hubeba maana kutegemea kichocheo, nia ya mtoaji wa lakabu na mandhari au mazingira ya anayepewa lakabu fulani. Madai haya yanaoana na ya watafiti kama vile Hang`ombe (2015) na Kabaso (2016) wanaosisitiza kwamba jina hutazamwa kama ujumbe ambao mtoaji wa jina hilo anataka kuelekeza kwa jamii kupitia kwa anayeitwa jina hilo. Lakabu,

kama yalivyo majina mengine halisi ni hifadhi ya hati ambamo mtu anaweza kusoma historia ya wanajamii katika nyakati mbalimbali. Zawawi (1998) anaeleza kuwa majina ya watu ni kigezo muhimu cha kuwatambulisha kitamaduni. Pia huwa na wajibu wa kisaikolojia wa kumtambulisha mtu. Majina huwasilisha tajriba za kitamaduni na kijamii za watu waliotunga majina hayo zaidi ya yote husawirisha namna wanajamii wanavyojistahi. Majina ni vioo vya maadili, utamaduni, tajriba na matukio katika maisha ya watu.

Kulingana na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti huu ni wazi kuwa majina ya lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda yana maana iliyowazi na pia maana batini ambayo inaegemea katika utamaduni wa jamii. Kila lakabu huashiria kitu katika dunia au muktadha wa matumizi kwa kuwa huwasilisha maana fulani wazi na pia maana fulani fiche kwa anayebuni lakabu au kutumia lakabu hiyo (Butoma 2009). Yule anayejipachika au kumpachika mwingine lakabu huwa na nia au shabaha itakayoafikiwa na lakabu hii. Uchanganuzi wa kisemantiki wa matokeo ya utafiti huu ulidhihirisha kuwa kwa kurejelea mihimili ya nadharia ya kisemantiki ya fremu pamoja na dhana za kisemantiki; maana wazi na maana halisi ya lakabu za wachezaji kandanda za EkeGusii, tunaweza kupata fremu muhimu zinazosaidia kueleza maana kwa njia sahili.

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa wachezaji kandanda wa jamii ya AbaGusii wana lakabu ambazo wao hutumia sambamba na majina yao halisia. Lakabu hizi zimeonyesha kuwa na maumbo mahususi pamoja na semantiki. Hivyo basi lakabu ni ishara ya kiisimu na hivyo basi inaweza ikachanganuliwa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Kwa kurejelea semantiki, utafiti umeonyesha kuwa lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda zina maana. Ili kueleza maana za lakabu hizi, utafiti huu ulitumia mihimili ya nadharia ya kisemantiki ya fremu inayoeleza kuwa maana ya neno inaweza kueleweka kwa kurejelea vielelezo vilivyomo akilini mwa mtu ambavyo vinatokana na uzoevu wa siku nyingi. Kulingana na waasisi wa nadharia hii, maana hutokana na maarifa yaliyohifadhiwa katika akili

kwa muda mrefu. Maarifa haya ndiyo yaliyotumika kufafanua maana za lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda. Fillmore (1985) anaeleza kwamba nadharia ya semantiki ya fremu hujaribu kufafanua maana ya neno kwa kulihusisha neno hili na usuli wake kwa jumla.

Lugha huonyesha utamaduni wa jamii fulani hivyo basi inaweza kueleweka kwa kurejelea upataji wa lugha fulani na pia mifanyiko kwenye akili ya mtu. Fremu ilitumika katika utafiti huu kuhushisha ujuzi wa utamaduni na dhana akilini. Kwa kutumia mhimili wa fremu utafiti huu uliweza kuweka lakabu katika makundi tofautitofauti kutegemea semantiki na usuli wa lakabu hizi. Kategoria hizi ni kama zifuatazo: lakabu zinazoonyesha maumbile na rangi, zinazowasilisha sifa mbalimbali, za wanyama wa kufugwa , mwituni na wa majini, za ndege na wadudu, za mimea, zinazoonyesha matendo fulani, zinazoonyesha vitu mbalimbali, zinazoonyesha umilikaji na za sehemu mbalimbali.

Kupitia kwa uchanganuzi wa kisemantiki wa matokeo ya utafiti, fremu muhimu ziliweza kupatikana zilizosaidia kueleza maana za lakabu kwa njia sahili. Fremu ni mfumo wa dhana ambazo zinahusiana kiasi kwamba ili kuelewa moja ya dhana hizi inakubidi kuelewa mfumo mzima unaohusishwa na dhana iliyotajwa. Hivyo imedhihirika wazi kuwa majina ya lakabu za EkeGusii ya wachezaji kadanda yana maana fulani wazi (tambuzi) na fiche (ashirifu) kwa anayebuni lakabu au kutumia lakabu hiyo.

Utafiti huu umefafanua mbinu mbalimbali zilizotumika katika kuunda lakabu mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa kuna mbinu kadha wa kadha zilizotumika katika uundaji wa lakabu mbalimbali. Baadhi ya lakabu zilizochanganuliwa katika utafiti huu ziliudwa kutokana na nomino mbalimbali zinazorejelea mahali, sehemu za mwili, majina ya wanyama wa majini na wa mwituni, majina ya wadudu, ndege, mimea na vitu mbalimbali. Lakabu nyingine ziliundwa kutokana na vitenzi mbalimbali vinavyochukua viambishi awali vya nafsi na hivyo kuainiswa katika kikundi cha kwanza cha nomino. Viambishi awali vilivyotumika sana katika uundaji wa lakabu ni vya kikundi cha 1 na 3/omo-/ kikundi cha

5/eri-/ , 6/ama-/ na 7/eke- /kikundi cha 9/e-/ , 9a/e-n-/ , 10/oro-/ , 12/ aka-/ , 21/na-/ Kiambishi awali /aka-/ cha kikundi cha 12 kinatumika kuleta dhana ya kumdhalilisha aliyebandikwa lakabu hiyo.

Lakabu nyingi zilizoainishwa katika utafiti huu zinachukua viambishi awali vinavyoonyesha hali ya umoja. Hii ni kutokana na sababu kuwa lakabu huwa mtu anabandikwa au akajibandika lakabu yeye mwenyewe. Ni kwa nadra sana utapata lakabu ikirejelea makundi. Kila mwanadamu ana sifa za kipekee zinazomtofautisha na mtu mwingine, upekee huu wa mtu ndio chanzo za lakabu mbalimbali. Mbinu nyingine zilizotumika kuunda nomino ni ukopaji, uradidi, ufupishaji na uhamishaji. Majina yaliyokopwa na ambayo yalitumiwa katika utafiti huu yalikuwa kutoka lugha ya Kiswahili. Utohozi ulitumika kubadili maumbo ya majina haya ya lakabu yaliyokopwa kuweza kuendelezwa kwa lugha ya EkeGusii.

Mbinu ya uradidi iliyotumika ni uradidi kamili uliochangia kusesitiza kwa maana iliyokusudiwa na lakabu husika. Mbinu ya ufupishaji iliyotumika ni ufupishaji mkato unaohusisha kudodoshwa kwa baadhi ya maneno katika jina ili kulifanya jina hilo kutamkika kwa urahisi. Lakabu nyingi zilizotumika katika utafiti huu ziliundwa kwa kutumia mbinu ya uhamishaji wa maana. Uundaji huu wa lakabu umedhihirisha kuwa lakabu ni ishara muhimu ya kiisimu na hivyo basi inaweza kuainishwa kiisimu.

Matokeo ya utafiti huu pia yalionesha kuwa maana iliyodhihirika katika lakabu za EkeGusii za wachezaji kadanda zina umuhimu katika mchakato wa mpira wa kandanda kwa sababu hupasha ujumbe kuhusu aliyetunga lakabu, anayerejelewa na lakabu hiyo na jamii ambayo imebuni lakabu hiyo. Lakabu, sawa na yalivyo majina halisi ya mtu, ni hati ambazo zinaweza kutumika kufafanua historia ya mtu katika kipindi maalimu cha maisha yake. Utafiti pia umeonyesha kuwa kuna uhusiano kati ya lakabu na wasifu au maumbile ya anayerejelewa na lakabu fulani. Lakabu huonyesha vipengele muhimu vya utamaduni wa mwafrika hivyo basi lakabu huweza kumtambulisha mtu na pia huweza kupitisha ujumbe muhimu kwa wale wanaoelewa maana na usuli wa lakabu hii pamoja na tajriba za utamaduni wa wanajamii waliobuni lakabu hizi.

Kutokana na data iliyoainishwa imedhihirika kuwa matumizi ya lakabu huathiri wachezaji wa kandanda kwa njia mbalimbali kutegemea kiini cha mashabiki kutumia lakabu fulani. Iwapo lakabu zinazotumika ni za kukejeli, kudhalilisha au kukashifu tabia fulani hasi wachezaji hawa hujikakamua na kutia bidii kujirekebisha ili kuepuka kutemwa kutoka kwenye timu. Iwapo lakabu zilizotumika ni za kusifu au za kujasirisha pia huwaathiri wachezaji kwa sababu huwapa hamasa kuendelea kutia bidii ili wasipoteze mnato wa mashabiki wao na pia waendeleo kuchezea timu zao katika nafasi walizopewa kwa sababu mchezo wa kandanda unahitaji bidii, mazoezi, ushirikiano, ustahimilifu na ustadi la sivyo mchezaji anaweza kupoteza umaarufu wake katika timu. Hii inaweza kuchangia mchezaji huyu kupoteza kipato chake pale ambapo anapoteza nafasi yake katika timu.

Utafiti umeonyesha kuwa lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda zilishamiri mafunzo kuhusu misimamo wa AbaGusii kuhusu maswala ya jinsia, kilimo, ufugaji na maadili kwa ujumla. Pia imedhihirika kuwa baadhi ya lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda zimekubalika kama majina asilia ya watu hasa lakabu zinazorejelea wachezaji mashuhuri katika jamii. Matokeo haya yanaoana na matokeo ya mtafiti Felecan (2009) anayesadiki kuwa wakati mwingine lakabu hurasimishwa na kuchukua nafasi ya majina asilia hasa pale ambapo majina haya asilia hayaonekani kumvumisha mtu jinsi anavyotaka

Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa matumizi ya majina ya lakabu ni muhimu sana kwa sababu yanapitisha ujumbe kwa jamii kuhusu anayebuni lakabu, anayerejelewa na lakabu na jamii ambayo imeunda lakabu hiyo. Lakabu hueleza hadithi kumhusu yule aliyebandikwa lakabu hiyo. Lakabu hufurahisha na utumika kuwatania na pia kuwafundisha watu. Lakabu hutumika kuwapa mawaidha watu kuhusu maswala ibuka yanayowaathiri watu katika jamii.

Utafiti huu umeonyesha kuwa lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda hutumika peupe bila kuficha hata kama ni za kukejeli au kusifia mchezaji. Matokeo haya ni kinyume na matokeo yake Felecan (2009) aliyedai kuwa lakabu hutania mrejelewa wa lakabu hiyo hivyo hutumika kisiri au wakati wa ugomvi.

Mwisho, utafiti huu umeonyesha kuwa lakabu za EkeGusii za wachezaji kandanda zina maana inayotokana na kichocheo cha utunzi wa lakabu hiyo, dhamira ya anayebuni lakabu hiyo na mandhari au hali ya anayerejelewa na lakabu fulani. Utafiti huu umejaribu kuainisha lakabu kwa kuangalia dhana za kisemantiki na maumbo ya lakabu hizi na umuhimu wake kitamaduni na kijamii kinyume na nyingi za tafiti zinazohusu lakabu za wachezaji kandanda ambazo huorodhesha lakabu ili kuziratibu.

5.3 Masuala yanayohitaji tafiti zaidi

Utafiti huu umeangazia masuala mengi muhimu kuhusu lakabu za EkeGusii: kisemantiki, kimatumizi, kimafundisho, kitamaduni na kijamii. Hata hivyo kuna mengi sana kuhusiana na lakabu za EkeGusii ambazo hazijajadiliwa katika utafiti huu. Hivyo basi ni muhimu kupendekeza yafuatayo kwa watafiti watakaovutiwa na tafiti zinazohusiana na utafiti huu wa sasa.

5.3.1 Kwa kurejelea matokeo ya utafiti huu kuna haja ya tafiti zaidi za kiisimu kuhusu lakabu katika lugha ya EkeGusii kwa sababu utafiti huu wa sasa hautoshi kuchanganua maswala yote ya kiisimu kuhusu lakabu kikamilifu.

5.3.2 Utafiti zaidi kuhusu lakabu unahitajika kufanywa hasa kutathimini iwapo wachezaji kandanda wanawake hubandikwa lakabu na iwapo lakabu zao zinalingana na hizi za wachezaji wa kiume zilizotumika katika utafiti huu.

5.3.3 Pendekezo lingine ni kuwa kuna haja ya waitifati kutafiti kuhusu lakabu za lugha ya EkeGusii na lugha zingine za kiafrika zinazotumika katika sajili ya michezo mbalimbali kama vile mchezo wa mpira wa vikapu, riadha na michezo mingineo.

MAREJEO

- Aboh, R. (2011). *Linguistic Construction of Identity and Politics in Selected Twenty First Century Nigerian Novels*. Staff/Post Graduate seminar series, Department of English, University of Ibadan.
- Abrahamsons, M. (1983). *Social Research Methods*. Englewood Cliff: Prentice-Hall.
- Ajileye, M. K. & Ajaleye, S. S. (1997). "Pragmasociolinguistic Features of Yoruba Nicknames" In B. Lawal (Ed), *Stylistics in Theory and Practice*. Ilorin: Paragon Books 195-204
- Bosire, K. M. & Machogu, K.G. (2013). *EkeGusii Dictionary*. Kenya; Ekegusii Encyclopedia Project
- Bowern, C. (2008). *Linguistic Fieldwork: A practical Course*. New York: Palgrave Macmillian
- Bickman, L. & Debra, J. R. (2009). *Applied Social Research*. London: Sage Publications.
- Buliba, A. S. Gwachi, J. M. & Matinde, S. R. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Tanzania: Serengeti Educational Publishers T LTD.
- Candrea, I. (2001). *Romanians and Nicknames*. (First edition appeared in 1985, in Bucharest, Socecu &Comp. Bookstore Publishing House.
- Cammenga, J. (2002). *Phonology and Morphology of EkeGusii; A Bantu Language of Kenya*. Koln: Rudiger Koppe Verlag.
- Chelliah, L. S. & Reuse, W, (2011). *Handbook of Descriptive Linguistic Fieldwork*. New York: Springer.
- Cooper, J. & Vaux, B. (2003). *Introduction to linguistic Field Methods*. Lincom Gmbh: Lincom Europa
- Corbin, J. & Strauss, A. L. (1998). *Basics of Qualitative Research (2nd edn)*. Thousand Oaks CA: Sage Publications

- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. New York: Oxford University Press.
- Dey, I. (1993). *Qualitative Data Analysis*. London: Routledge
- Fasold, R. (1990). *The Sociolinguistic of Language*. Oxford University Press
- Felecan, D. (2009) “Nicknames-AReflection of Polyphony within the Linguistic Area from the Northwestern part of Romania” *Nomina African, VOL 23 No 2pp 61-90*.
- Felecan, O. (2012). *Name and Naming: Synchronic and Diachronic Perspective*.New Castle; Cambridge scholars publishing.
- Fillmore, C.J. & Collins F. B. (2001). “*Frame Semantics of Text Understanding*” Proceedings of Wordnet and other Lexical Resources Workshop. Naacl.
- Graur, A.L (1965). Nicknames.*In Numes de personae (Personal Names) PP 70-72* Bucharest: Editura Stiintifica (Scientific Publishing House).
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hjerstedt, I. (1987). *Middle English Nicknames in the Lay Subsidy Rolls for Warwickshire*.Uppsala; University of Uppsala.
- Ibuken, F. & Omotosha, M. M. (2014). *A Social-Semiotic study of nicknaming among Undergraduates in Nigeria*. Ibadan: Nigeria.<http://dx.org/10/3092/10.681632>. Accessed apri.22 2017
- Johnstone, K. (2008). *Quantitative Methods in Linguistic*. Wiley: Blackwell
- Ladefoged, P. (2003). *Phonetic Data Analysis: An Introduction to Fieldwork and Instrumental Technigues*. Oxford: Blackwell publishing.

Lakaw, A. (2006). *Hiding Behind Nicknames: a linguistic study of Anonymity in IRC Chatrooms* student thesis. Vaxjo University. <http://nu.diva-portal.org/Smash/record/sf?PID=diva2:206935>, accessed sept 11, 2015.

Lyons, J. (1977). *Semantics*. Cambridge: University Press

Kahari, G. (1990). *Plots and Characters in Shona Fiction*. Gweru: Mambo Press.

Kennedy, R. & Zamuner, T. (2001). *Nicknames and the Lexicon of Sport*. Santa Barbara; University of California.

Kenya National Bureau of Statistics (2010). 2009 Kenya Population and Housing Census: Population and distribution by age, sex and administrative units (Volume 1c) Nairobi: Government press.

Kenya National Bureau of Statistics (2019). 2019 Kenya Population and Housing Census: Population by County and Sub-County (Volume 1) Nairobi: Government press.

Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology; Methods and Techniques, 2nd Edition*, New Delhi; New Age International (P) Limited Publishers

Maina, J. (2015). Cruel Nicknames Tell Many Tales. Nairobi: *The standard Newspaper*. 5th Feb. 2015.

Malande, J.O.M. (2011). What's in a Name? An Analysis of the Semantics of Lulogooli Personal Nouns. *International Journal of Humanities and Social Sciences* 1(20), pp 211-218

Maho, J. F. (2008). *The Bantu Bibliography (African linguistic bibliography)* Koln: Rudiger Koppe Verlag.

Mashiri, P. (2004). *More Than Mere Linguistic Tricks: The Socio-Pragmatic Functions of Some Nicknames used by Shona-Speaking People in Harare*. Harare: Zambezia. University of Zimbabwe.

- Mason, M. (2010). *Sample Size and Saturation in PhD Studies Using Qualitative Interviews*. *Forum: Qualitative Social Research* 11(3)8. Retrived from <http://qualitative-research.net/index.php/fqs/article/view/1428/3027>
- Massamba, D. P.B (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matel, K.A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi Kwa Shule za Upili*. Kenya: Oxford University press.
- Matinde, S. R. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo Vya Kati na Vyuo Vikuu*. Tanzania: Serengeti Educational Publishers T LTD.
- McDowell, J. H. (1981). Towards a semiotic of nicknaming: The Kamasa example” *Journal of American folklore* 94:1-18.
- Mdee, S. et al (2011). *Kamusi ya Karne ya 21: Kamusi ya Yenye Ukeketo Zaidi Katika Karne hii*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) LTD.
- Mgullu, R. S (2002). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn
- Mose, E. Mwangi, P. & Njoroge, M. (2013). Harmonizing the Orthographies of Bantu Languages: The case of Gikuyu and Ekegusii in Kenya. *University of Nairobi Journal of Language and Linguistic*. Vol 3 PP 109-121.
- Newman, P. & Ratliff, M. (2001). *Linguistic Fieldwork*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Nurse, D. & Philipson, G. (1980) *The Bantu Language*. London: Routledge.
- Nyakundi, P. M. (2010). *Motivational, Morphological Process in Egesembea Argot EkeGusii Speaking Males of Western Kenya*. (Unpublished Masters thesis) Kenyatta University, Nairobi. Kenya.

- Obuchi, S.M. & Mkhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A flame Publishers.
- Odoch, P.J. P. (2017). Indigenous Knowledge in Acholi Nicknames. Nairobi: *Regional Journal of Information and Knowledge Management*, 2 (2),1-13.
- Phafoli, L. (2009). Naming Among Basotho Accordion Artists: *In Nomina Africana (2009) Volume 23 (1); 91-112*
- Sebastian, L. (2014) “Evidence for frames from Human Language in T. Gomerschlag, D. Gerland, R. Osswald & W. Petersen, (edi.), *Frame and Concept Types*, PP 23-67, Springer, Dordrecht.
- Taylor, L. P. (2011). *Objectionable Team Nicknames: Determining the Likelihood of Selling the Issue of Banning Them in Virginia High schools*. Phd Thesis. Viginia. Commonwealth University
- Trask, R. I. & Stockwell, P. (2007). *Language and linguistic: The key concepts (2nd Ed.)* New York. Routledge.
- Wainaina, N. (2013). How Nicknames Helped Central Politician Win. Nairobi: *The Stardard Newspaper*. 5th Apr. 2013.
- Watts, M. (2006). In Search of the Holy Grail: Project Proposals and Research Design, but Mostly about Why Writing a Dissertation Proposal is so difficult. In E. Perecman & S.R. Curran (Eds). *A Handbook for Social Sciences Field Research Essays & Bibliographic Sources On Research Design and Methods*. (175-197) London: Sage Publications.
- Yule, G. (1993). *The Study of Language*. London: Cambridge University Press.